**WAZIRI** Utumishi aagiza uchunguzi wa kesi za 'kumalizana' ujauzito

UKURASA 2



**MUUGUZI** apandishwa kortini kwa tuhuma rushwa ya 200,000/-

UKURASA 3


Polepole na mjadala wa kurefusha urais wa JPM

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

NI OTHAM MASOUD

UCHAMBUZI

Kifo cha Seif kilivyoyozima ndoto za Profesa Lipumba

Aambiwa aache kumwota Hamad aangalie wengine

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Machi 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580508

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# TCRA yatangaza neema kwa watumiaji wa simu

**KIAMA** kwa wale wa 'tuma kwa namba hii' chawadia...*Endelea Uk. 2*



## OTHMAN ABAINISHA MAMBO 3 YALIYOMBEBA

UKURASA 3

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Othman Masoud Sharif kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Ikulu jana. **PICHA: IKULU**

## Saudia yatoa masharti Hija, Mufti atoa kauli

UKURASA 19

**MICHEZO** **LUKAKU APOTEZEA MBIO KIATU NA RONALDO SERIE A** UK. 21

**MAONI, KATUNI UK. 6**

## HABARI KITAIFA

# TCRA yatangaza neema kwa watumiaji wa simu

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imetoa mwongozo wa kanuni ndogo 12 zinazolenga kutatua kero za watumiaji wa huduma simu ikiwamo matumizi ya vifurushi zitakazoanza kutumika rasmi Aprili Mosi mwaka huu.

Hatua hiyo imekuja baada ya mamlaka hiyo kupokea jumla ya maoni 3,278 ya malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali ikijumuisha watumiaji, watoa huduma, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ili kutatua kero na kuongeza ustawi wa Sekta ya Mawasiliano.

Mkurungezi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, alisema kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau, mamlaka hiyo wameandaa kanuni hizo ikiwamo ya mtoa huduma hataruhusiwa kutoa kufanya shughuli hizo bila kibali cha mamlaka.

Alitaja kanuni nyingine kuwa ni mtoa huduma ataweka utaratibu wa kumwezesha aliyejiunga na kifurushi chochote, kuendelea kutumia muda au uniti za kifurushi ambacho kitakuwa kimesalia ndani ya muda wa matumizi uliowekwa kwa kununua tena kifurushi hicho hicho kabla ya kumalizika muda wake.

Vilevile, alisema mtoa huduma ataweka utaratibu au mfumo wa kumwezesha mtumiaji wa huduma kuhamisha uniti za kifurushi kwenda kwa mtumiaji mwingine ndani ya mtandao wake kwa masharti yaliyopo.

"Masharti hayo ni kiasi kisichopungua MB 250 na mtumiaji anaweza kuwahamishia watumiaji wasiyozidi wawili na mtumiaji aliyehamishiwa uniti za kifurushi hataruhusiwa kumhamishia mtumiaji mwingine uniti hizo au sehemu ya uniti alizohamishiwa," Kilaba alifafanua.

Alisema mtoa huduma atapaswa kuhakikisha kwamba bei za vifurushi zinazingatia bei husika ya chini na ya juu zilizowekwa na mamlaka pamoja na kutumia lugha rahisi na vigezo na masharti yaliyo wazi kuhusu vifurushi vinavyotolewa.

Vilevile, alisema vifurushi vinavyotolewa kwa mtumiaji havitaondolewa, havitarekebishwa au kubadilishwa ndani ya miezi mitatu baada ya kuidhinishwa.

Kadhalika, alisema mtoa huduma ataweka utaratibu au mfumo wa kumwezesha mtumiaji wa huduma mwenye simu janja, kufuatilia matumizi ya data kwa kupakua programu ya mtoa huduma.

Pia, alisema mtoa huduma hataruhusiwa kupunguza kasi ya data kwenye kifurushi cha mteja ndani ya muda wa kifurushi husika na hatafanya promosheni zaidi ya tatu au kutoa ofa maalum zaidi ya tatu kwa wakati mmoja kupitia huduma za sauti, ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) na data.

Kilaba alisema kanuni hizo zitakapoanza kutumika, zitasaidia kujibu malalamiko mengi ya wateja kwa sasa na kusisitiza watumiaji kuendelea kufuatilia mabadiliko hayo kwa umakini na kwa mtazamo chanya.

"Kanuni hizi zitaboresha huduma za vifurushi kutokana na maoni ya wengi kuwa vifurushi vimekuwa vikiwasaidia," alisema.

Katika hatua nyingine, Kilaba aliwataka Watanzania kuendeleza kupambana na masuala ya utapeli mtandaoni na kuwataka kuendelea kusoma mwongozo wa TCRA kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano.

"Usikubali kutapeliwa kwa kutekeleza maelekezo yanayohusu muamala wowote wa kifedha katika simu yako kwa kupigiwa simu na mtu yeyote anayejifanya mfanyakazi wa kampuni yoyote ya simu au wakala wake," alisema.

Kilaba alisema ikitokea mtumiaji wa simu amepigiwa simu au kutumiwa ujumbe mfupi wowote wa kitapeli, asiutekeleze badala yake autume ujumbe huo kwa namba 15040 na namba iliyomtumia ujumbe huo.



Balozi wa Ujerumani nchini, Regina Hess (kushoto) na Mratibu wa Taasisi ya Utalii ya Old Moshi Cultural Tourism, Gabriel Mzei Orio, wakiweka mishumaa kwenye kaburi la Mangi Meli Makindara, katika eneo la Kolila, wilayani Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro jana, kuadhimisha kumbukizi ya shujaa huyo wa jamii ya Wachaga, aliyeuawa kwa kunyongwa na wakoloni wa Ujerumani, Machi 2, 1900. **PICHA: JAMES LANKA**

# TAKUKURU yakabidhiwa kesi wazazi kumalizana

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeagizwa kushughulikia kesi za mimba za utotoni ambazo zimekuwa zikiishia mitaani badala ya kwenda kwenye vyombo vya sheria.

Vilevile, imeagizwa kufanya utafiti kuhusu rushwa ya ngono kwa vyuo vikuu vingine na vyuo vya kawaida, kama ilivyofanyika kwa vyuo vikuu vya Dodoma (UDOM) na Dar es Salaam (UDSM) ili kutokomeza rushwa hiyo.

Maagizo hayo yalitolewa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora na Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Deogratius Ndejembi, alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa TAKUKURU wa kutathmini utendaji kazi kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2020.

Alisema amekuwa akishuhudia kesi kama hizo nyingi katika maeneo mbalimbali zikiishia mitaani, na kutaka taasisi hiyo ilivalie njuga suala hilo ili kuwashughulikia wanaofifisha ndoto za watoto.

"Unakuta kesi nyingi za mimba mnazifuatilia ama kuzipeleka mahakamani, lakini ikifikia mahakamani mhusika hatokei au anakana tukio, ukifuatilia unakuta wahusika wamemalizana mtaani kwa kulipana faini, jambo hilo halikubaliki," alisema Ndejembi.

Aliongeza: "Hii imekuwa ni desturi ya wazazi pale unapowakamata wahusika wao humalizana kesi na watendaji."

"Unakuta mwalimu amempa mimba mwanafunzi, lakini ukiifuatilia hiyo mwisho wa siku unakuta mtenda kosa yupo mtaani na ukiuliza unaambiwa alimazana na wazazi wa mwanafunzi.

"Ninaomba TAKUKURU mtusaidie kufuatilia suala hili kwa sababu linakuwa sugu na wahusika wanajisikia vibaya kuona watu wanaotenda makosa kama hayo wapo mtaani ilihali wao maisha yao yameharibika," alisema Ndejembi.

Alisema sheria ipo na hao wazazi wanaofanya vitendo hivyo wawajibishwe kwa mujibu wa sheria za nchi zinavyoelekeza ili hizo mimba za utotoni ziishe.

Alisisitiza wazazi kuhakikisha wanaacha vitendo hivyo kwa kuwa wanakatisha ndoto za watoto wao.

Ndejembi alisisitiza idara ya elimu, halmashauri zihakikishe kesi hizo zinazofanyiwa kazi na mamlaka mbalimbali ili kuhakikisha wanafunzi hao wanapata haki yao ya msingi ya kusoma.

Kuhusu rushwa ya ngono, alitaka TAKUKURU kuhakikisha inafanya utafiti wa rushwa hiyo hadi kwenye shule za msingi na sekondari.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema moja ya mikakati ambayo wamejiwekea ni kutekeleza ilani ikiwamo kusimamia mafanikio yao katika kupambana na rushwa.

# Babu afariki kwa kuzama kisimani

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MKAZI wa Kijiji cha Butairuka, Joseph Rutabana (74), amepoteza maisha baada ya kutumbukia katika kisima cha maji kilichochimbwa katika eneo la Kanisa Katoliki Parokia ya Maruku, wilayani Bukoba.

Mkaguzi Msaidizi Abrahman Ngaugia ambaye ni Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Bukoba, alisema tukio hilo lilitokea juzi na kwamba walipata taarifa ya kwenda kufanya uokoaji saa 10:04 alasiri.

"Baada ya kupokea taarifa, tulikwenda eneo la tukio kwa lengo la kuokoa maisha ya mzee huyo, lakini kwa bahati mbaya tulikuta amekwishapoteza maisha," alisema Ngaugia.

Alisema askari wa jeshi hilo, Sajenti Karata Ramadhan, ndiye aliyeingia katika shimo hilo na kuutoa mwili wa mzee huyo kwa kushirikiana na askari wenzake.

"Alitumbukia katika shimo la kisima chenye kina kirefu kati ya mita 30 na 35 kilichoko ndani ya eneo la kanisa. Tulifanya uokoaji kwa mara ya kwanza kwamba ikakatika kutokana na uzito na uwepo wa maji na tope katika shimo hilo. Lakini mara ya pili tulifanikiwa kutoa mwili wake," alisema.

Mwili huo, baada ya kutolewa umekabidhiwa kwa Jeshi la Polisi na baadaye kupelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa kwa ajili ya taratibu zingine.

Mkuu wa Parokia ya Maruku, Padri Hubert Muyerero, alisema akiwa amepumzika alipata taarifa kutoka kwa msaidizi wake kuwa kuna mtu ametumbukia katika kisima cha maji. Baada ya kupokea taarifa hizo alipiga simu polisi ambao walifika haraka wakiwa na askari wa zimamoto na uokoaji.

Alisema katika eneo hilo kuna mafundi ujenzi walikuwa wakiendelea na shughuli zao na kwamba ndiyo waliomwona akihangaika kuondoa mfuniko ili aingie katika kisima hicho lakini kwa bahati mbaya walikuwa wamepanda juu hivyo hawakuwahi kumwokoa.

Mmoja wa ndugu wa marehemu, Anadetha Bayekera, alisema ndugu yao aliondoka nyumbani na kuaga kwamba anakwenda kuoga baada ya hapo hakuonekana tena hadi walipopewa taarifa za tukio hilo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Butairuka, Arbogast Bandiho, alisema siku chache kabla ya tukio mzee huyo alionekana kuchanganyikiwa na kwamba inawezekana tatizo hilo ndilo limesababisha kuchukua uamuzi huo.

HABARI KITAIFA

# Othman ataja mambo 3 makuu yaliyombeba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**



MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Sharif, ametaja mambo matatu anayohisi kumsaidia kuteuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kushika nafasi hiyo.

Othman aliapishwa rasmi jana na Rais Dk. Mwinyi, Ikulu ya Zanzibar, kushika nafasi hiyo baada ya kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Seif Sharif Hamad.

Akizungumza na waandishi wa habari, Othman alitaja mambo hayo kuwa ni uzoefu katika kazi, kufanya kazi kwa ushirikiano na muumini wa kutaka nchi kuwa mbali zaidi kimaendeleo kuliko ilipo sasa.

Alisema pia ana uzoefu mkubwa katika ngazi ya kimataifa ya namna ya kusimamia taasisi za umma na kuziendesha.

Akizungumzia kuendeleza maono ya Maalim Seif kuhusu umoja, alisema ataendeleza umoja na maridhiano yaliosimamiwa na Maalim Seif na kwamba nchi haiwezi kuendelea bila kuwa na umoja.

“Mimi ni muumini wa umoja kwa sababu naelewa umuhimu wake, ugomvi wa Wazanzibari ni wa kubuni hivyo suala la umoja ni muhimu kwa maendeleo ya Wazanzibari,” alisema.

Alisema nafasi ya umakamu wa kwanza ni wajibu wa kikatiba na kwamba sio rahisi kuwapo mtu atakayefanana na Maalim Seif.

Alisema atamsaidia Rais kujenga Zanzibar katika msingi imara wa maridhiano, kutazama maslahi mapana ya taifa na matarajio ya wananchi.

“Sote ni mashahidi tumetumia muda mwingi kwa mambo ambayo hayajatupeleka mbele pale panapostahiki kwa hivyo kwa kutumia uzoefu niloupata nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kumsaidia Rais kujenga msingi madhubuti, yeye kwa kushirikiana na mzee wetu Maalim Seif waliujenga ukiwamo wa maridhiano,” alisema.

Alisema bila ya kuwa na serikali madhubuti haiwezekani kuwa na sera na sheria imara, usimamizi bora wa sheria na huduma nzuri kwa wananchi na kuahidi kuimarisha misingi ya uwajibikaji, weledi na kutengeneza sera na sheria bora kwa maendeleo ya kiuchumi na kimaendeleo.

“Kujenga misingi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuifanya serikali ya kuwahudumia wananchi na kujenga serikali ambayo itasimamia maridhiano endelevu na amani na utulivu katika nchi yetu,” alisema.

Baada ya hafla ya kiapo hicho, Othman alizungumza na wananchi na wafuasi wa Chama cha ACT-Wazalendo katika ofisi za chama hicho zilipo Vuga na kuwaambia mzigo aliotwishwa wa umakamu wa kwanza wa rais ni mzito na kuwaomba ushirikiano.

Alisema maisha ya Maalim Seif ni sawa na kitabu na kimesomwa na watu wote ambayo ni urithi mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wake Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema chama anachokiongoza kimempata mrithi wa Maalim Seif bila ya kukwaruzana.

Alisema watahakikisha wanaendeleza mawazo na fikra za Maalim Seif kwa maendeleo ya chama na wananchi wa Zanzibar.

Hafla ya kiapo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali na vyama vya siasa.

# Muuguzi kortini madai ya rushwa

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, Tabora, imempandisha kizimbani mkazi wa mtaa wa Masanga, Wallace Kazili (52) kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Kazili, ambaye ni mtumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga, alifikishwa juzi katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa mgonjwa.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Wilaya ya Igunga, Mazengo Joseph, alidai kwamba mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo kinyume na kifungu cha 15 (1) (a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya Lyidia Ilunda, Joseph alidai kwamba mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo Oktoba 30, 2019 akiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga.

Alidai kuwa akiwa muuguzi, Kazili aliomba rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa Kazembe Bundala Nangale ili ampatie kumpatia dawa za kifua kikuu (TB) mama yake aliyekuwa amelazwa katika hospitali ya wilaya.

Pia mwendesha mashtaka alidai kwamba katika tarehe hiyo hiyo, mshtakiwa alipokea kwa njia ya simu Sh. 50,000 kama sehemu ya malipo ya awali Sh. 200,000 alizoomba.

Sambamba na hayo, alidai kuwa Novemba 1, 2019, mshtakiwa alipokea tena Sh. 50,000 kama sehemu ya malipo mengine, hivyo kufanya jumla ya fedha alizopokea kuwa Sh. 100,000.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa alikana kutenda makosa hayo na kudai kuwa wakili wake hayupo. Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana ya Sh. 300,000 za maandishi hadi Aprili 28, mwaka huu, kesi itakapotajwa.



ARIPO African Regional Intellectual Property Organization

**CALL FOR EXPRESSION OF INTEREST CONSULTANCY FOR ORGANISATIONAL REVIEW AND JOB RECLASSIFICATION**

The African Regional Intellectual Property Organization (ARIPO) is an Intergovernmental Organization created in 1976 under the Lusaka Agreement concluded under the auspices of the United Nations Economic Commission for Africa (UNECA) and the World Intellectual Property Organization (WIPO). Membership of the organization is open to all members of the African Union (AU) or of the United Nations Economic Commission for Africa (UNECA). The present members of the Organization are: Botswana, The Gambia, Ghana, Kenya, Lesotho, Liberia, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Rwanda, Sao Tome and Principe, Sierra Leone, Somalia, Sudan, Swaziland, Uganda, United Republic of Tanzania, Zambia and Zimbabwe. (Total: 20 Member States)

ARIPO wishes to conduct an organizational review and job reclassification exercise for the encumbered positions in the Organization as part of periodic organizational planning and review. Therefore ARIPO seeks to engage a Consultant from any part of the world to undertake organisational review and job reclassification in accordance with the International Civil Service Commission standards. The assignment shall involve benchmarking with other analogous Regional and International/Intergovernmental Organizations.

The Consultant should possess a relevant Bachelor's and Master's Degree with at least ten (10) years' proven organizational review and job reclassification experience in Intergovernmental Organizations and must not be a staff member of any of the governing bodies of ARIPO. The Consultant can be an individual or a body corporate. In the case of body corporates, the firm shall be evaluated based on the Lead Consultant's qualifications.

Interested Consultants are invited to obtain the Terms of Reference (ToRs) from ARIPO by contacting the Secretariat by email at **mail@aripo.org** with the reference on the subject: "Organizational Review and Job Reclassification".

Deadline: Submissions of proposals shall be by email not later than March 9, 2021. This call is not restricted to Consultants/Firms from the ARIPO Member States.

**A: 11 Natal Road, Belgravia, P.O. Box 4228, Harare, Zimbabwe,**
**T: +263 4 794 065/6/8/54/74 I +263 731 020 609, F: +263 4 794 072,**
**E: mail@aripo.org, W: www.aripo.org**

# Wananchi walia umeme kukatika mara kwa mara

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Manispaa ya Kahama mjini mkoani Shinyanga wamelalamika kukatika kwa umeme kila mara na kusababisha shughuli za uzalishaji mali katika viwanda kusimama.

Mmiliki wa mashine ya kuchakata mpunga, George Makula, alisema jana kuwa wiki iliyopita umeme ulikuwa unakatwa saa tatu asubuhi na kurejeshwa saa nne usiku na kusababisha kusimamisha shughuli za uzalishaji.

Alisema wameanza kujipanga ili wanunue jenereta kukabiliana na hali hiyo kuhakikisha kazi zao hazisimami.

Denis Kasindi, mkazi wa Nyahanga, alisema baadhi ya wafanyabiashara wameingia kwenye mikopo na taasisi za kifedha, hivyo umeme unapokatika bila kutoa taarifa, unasimamisha uzalishaji na kuwaweka hatarini kushindwa kulipa mikopo husika.

Kasindi alisema taarifa ambazo zimekuwa zikitolewa kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha umeme umekuwa ukikatika maeneo ya Isaka, Mwakata, Nhumbi, Kagongwa, Mondo, Mwendakulima, Nyakato, Mwime, Mhungula, Shunu, Manzese, Lugela, Bukondamoyo, Halmashauri ya Ushetu na baadhi ya maeneo ya Nyahanga.

"Siyo wateja wote wana uwezo wa kuingia kwenye makundi ya WhatsApp ya Tanesco kuangalia ratiba ya kukatika kwa umeme, kama wanaendelea na kurekebisha mifumo yao ya umeme, ni vema wakatutaarifu siku mbili kabla kama wanavyofanya Mamlaka ya Maji (KUWASA) wakati wa marekebisho ya mifumo ya maji," alishauri.

Neema Tabu, mkazi mwingine wa halmashauri hiyo, alisema kipindi cha nyuma wakati umeme umeunganishwa katika kituo cha umeme kilichoko Mgodi wa Buzwagi, ulikuwa haukatiki kama ilivyo sasa.

Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) wilayani Kahama, King Fokanya, alisema suala hilo lipo nje ya uwezo wake na kwamba tatizo hilo linaanzia mjini Shinyanga.



Mjasiriamali wa kampuni ya Jiko Matawi, Fatuma Mganga (kulia), akifuta vumbi majiko yake, katika maonyesho ya wiki ya viwanda kwa wanawake yaliyoandaliwa na Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), kwenye viwanja vya Kijitonyama, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madarasa 2,200 yajengwa miezi miwili

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

VYUMBA vya madarasa 2,257 vimejengwa ndani ya miezi miwili ili kuchukua wanafunzi 74,166 wenye sifa za kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 ambao hawakupangiwa shule katika awamu ya kwanza.

Ujenzi huo ulitokana na agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, la Desemba mwaka jana kwa wakuu wa mikoa kuhusu namna ya kupokea wanafunzi hao.

Majaliwa aliwaagiza wakuu wa mikoa wote kuhakikisha wanafunzi wenye sifa za kujiunga na kidato cha kwanza ambao hawakupangiwa shule katika awamu ya kwanza, wanapata nafasi ifikapo Februari 28, mwaka huu.

Akitoa taarifa maalum ya utekelezaji wa agizo hilo jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema madarasa yaliyohitajika kwa ajili ya wanafunzi hao ni 1,484, lakini yamejengwa mengine ya ziada 773 na kuwa 2,257.

"Hadi kufikia Februari 28, mwaka huu, jumla ya vyumba 2,257 vimejengwa vikiwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 112, 850 kwa uwiano wa wanafunzi 50 kwa kila chumba cha darasa.

"Tungeweza kuchukua wanafunzi wengine kwa ziada ya vyumba hivyo tungekuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 38,684," alisema.

Aliagiza mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuanza kufanya maoteo ya wanafunzi watakaojiunga na elimu ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza kwa mwaka 2022 na maandalizi ya miundombinu na madawati kuanza mara moja.

"Ujenzi wa madarasa kwa mwaka 2022 usisubiri maelekezo ya serikali kuu. Viongozi wote wa mikoa na wilaya na wakurugenzi sasa waanze kufanya maoteo ya vijana ambao wanatarajiwa kupokewa mwakani kuanzia elimu ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza," aliagiza.

Jafo alisema serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya shule za sekondari na kutaka miundombinu hiyo ikamilike kabla ya uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na kidato cha tano 2021 utakaofanyika Mei, mwaka huu.

Aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa, kuhakikisha ujenzi wa mabweni, madarasa, maabara na matundu ya vyoo unakamilika haraka. "Serikali imeshapelekeza fedha huko, hatutarajii muda ukiwa umefika wa kuchagua wanafunzi wa kidato, miundombinu hiyo iwe haijakamilika," alionya.

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 130 wasoma darasa moja, waketi chini

**Na Dinna Maningo, TARIME**

ZAIDI ya wanafunzi 130 wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Buhemba, Kata ya Bomani wilayani Tarime mkoani Mara, wanalazimika kusoma kwenye chumba kimoja cha darasa huku wengine wakiketi chini kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Mbunge wa Tarime Mjini, Michael Kembaki, alipotembelea miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na barabara za mjini zinazotarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mbunge huyo aliongozana na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime ambaye ni Diwani wa Nyamisangura, Thobias Ghati.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Buhemba, Kordine Kivuyo, alisema darasa moja wanatakiwa kukaa wanafunzi wa awali 25, lakini kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa wanakaa 135.

"Darasa moja halitoshi kwa kuwa hakuna madarasa, wanalazimika kurundikana darasa moja, wanafunzi wa awali wanatakiwa kukaa 25 kwenye darasa moja na baadhi ya wanafunzi wanakaa chini na darasa halina sakafu.

"Wanabanana hivyo hivyo na inakuwa kero kwao na mwalimu anapata shida kufundisha ikizingatiwa kuwa ni watoto wadogo, wanahitaji mazingira rafiki ili iwe rahisi katika ufundishaji," alisema mwalimu huyo. Alisema shule yake ina wanafaunzi 1,400. Kati yao, wavulana ni 669 na wasichana 731, hivyo kuna uhitaji wa madarasa 32 lakini yaliyopo ni 14, madawati yanahitajika 482 lakini yaliyopo 291, matundu ya vyoo yanahitajika 64 na yaliyopo 10.

"Walimu wanaohitajika ni 32 lakini waliopo 24, nyumba za walimu zilizopo ni mbili, tunahitaji printa na mashine ya 'photocopy', madarasa matatu hayana sakafu, tumejitahidi kutatua baadhi ya changamoto kama ukarabati wa madawati.

"Tuna umeme ambao umetusaidia kupunguza gharama za uchapaji mitihani, tuna maji ya bomba na shamba la shule kwa ajili ya kilimo kinachowawezesha wanafunzi kupata maarifa," alisema.

Mbunge Kembaki aliahidi kufanya harambee ambayo ataalika wadau mbalimbali kuchangia fedha kujenga madarasa ili kuondokana na changamoto ya uhaba wa madarasa. "Bado tuna changamoto za kitaaluma kama upungufu wa walimu, vyumba vya madarasa, madawati na mahitaji mengine.

"Kwa kuwa mmenipa kazi ya kushawishi wananchi kuchangia maendeleo ya shule, nitafanya harambee tupate fedha na siku ya harambee nitawaletea printa.

"Nimefurahishwa mmejenga msingi wa vyumba vitatu vya madarasa, tena kwa gharama ndogo, kuna maeneo mengine misingi imejengwa kwa gharama kubwa," alisifu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Pipe Industries Ltd, Seif Ali Seif, akifafanua jambo kwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alipotembelea kiwanda hicho kilichoko Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Bandari ya uvuvi biashara kujengwa

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema imejipanga kuboresha sekta ya uvuvi kwa kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwamo kujenga bandari ya uvuvi ili kuboresha huduma kwa meli zinazofanya uvuvi wa kibiashara katika bahari hususani ukanda wa uchumi wa bahari kuu.

Akifungua mkutano wa wadau wa sekta hiyo jijini Dar es Salaam, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema ujenzi wa bandari hiyo unakusudia kuondoa changamoto za kukosekana kwa huduma za kushusha samaki waliolengwa na wasiolengwa.

Pia, alisema itasaidia katika ukaguzi wa samaki waliovuliwa, kuegesha na kufanya ukarabati wa meli, kupakia maji na chakula, mafuta pamoja na kushusha na kupakia mabaharia.

Alisema hatua za upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari hiyo zimekamilika kupitia mshauri mwelekezi kwa hatua za awali.

Ndaki alisema maboresho mengine ambayo yanafanyika katika sekta hiyo ni kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta ya hiyo.

Jingine alisema inaboresha tafiti zinazohusu rasilimali za uvuvi, kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za sekta hiyo, kusimamia na kuendeleza shughuli za ukuzaji viumbe maji na kuboresha huduma mbalimbali ikiwamo mafunzo, ugani, maabara, ushauri na mazingira ya biashara ya mazao ya uvuvi.

Alisema lengo la serikali kufanya uboreshaji huo ni kuhakikisha sekta hiyo inakua kwa kasi na kuongeza mchango wake katika pato la taifa tofauti na ilivyo kwa sasa.

Ndaki alisema katika kufufua TAFICO, itaandaa mpango wa biashara wenye maeneo matatu ikiwamo ya uvuvi wa bahari kuu, ufugaji samaki na uchakataji wa mazao ya uvuvi ambayo yatatekelezwa kupitia miradi midogo kumi kumi yenye thamani ya Sh. bilioni 89.3. Alisema miradi hiyo itahusisha kununua meli nne za uvuvi, mradi wa viwanda vya kuchakata samaki na ukuzaji wa viumbe maji.

Ndaki alisema tayari serikali imepata ufadhili kutoka Serikali ya Japan kupitia programu ya maendeleo ya uchumi na jamii wenye thamani ya Sh. bilioni 4.2 ambao sehemu ya fedha hizo itatumika katika ujenzi wa meli yenye urefu wa mita 22 itakayovua katika ukanda wa uchumi wa bahari.

Alisema msaada huo utahusisha usimikaji wa mitambo ya kuzalisha barafu na ujenzi wa ghala la baridi la kuhifadhia samaki.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, alisema bado rasilimali za uvuvi hazijatumika ipasavyo na kwamba kuna haja ya kuifanyia maboresho zaidi ili yalete matokeo chanya kwa wazalishaji wenyewe na kwa pato la taifa.

# Aweso atoa siku 7 kuondolewa mabomba yaliyotelekezwa

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametoa siku saba kuondolewa kwa mabomba ya maji yaliyotelekezwa kwenye kiwanda cha Pipe Industries Company cha jijini Dar es Salaam, yanayotakiwa kutumika kwenye mradi wa maji wa Bwiti Tandahimba mkoani Mtwara, ili kutatua changamoto ya maji.

Aweso ametoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kutembelewa viwanda vinavyotengeneza mabomba ya maji ambayo serikali imekuwa ikiyatumia katika miradi yake ya maji.

Alisema mradi huo wa maji unatakiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja matokeo yake hadi sasa una zaidi ya miaka mitatu haujakamilika na mabomba yamelipiwa katika kiwanda hicho.

"Hii ni moja ya changamoto na haya ni maelekezo mabomba yatolewa haraka yakafanye kazi na wananchi wapate maji unaweza kufanya ziara kule wakakueleza tumeagiza bidhaa ya mabomba bado hayajakamilika kumbe tayari yameshakamilika sasa yaondolewe dhamira yetu ni kumtoa mama ndoa ya maji kichwani," alisema Aweso.

Aliongezea kuwa "Tumeona kabisa eneo la mradi wa Bwiti mabomba yametekelezwa, lakini ukienda kwenye mradi wanasema kuna changamoto na fedha zimelipwa hii sio sawa wasichukue wiki mambo yawe yametolewa."

Alisema amejiridhisha utendaji kazi wa viwanda vinavyotengeneza mabomba ya maji nchini, huku akiwataka wataalamu wake kuacha kuwatumia vishoka katika miradi ya maji.

Aweso alisema atakwenda kushughulikia madeni ambayo serikali inadaiwa na kampuni zinazotengeneza mabomba walipwe kwa wakati.

"Sekta ya maji ni eneo nyeti na limebeba uhai kwa Watanzania ni sekta ambayo haina mbadala mtu akikosa maji anapata maradhi hivyo changamoto yake ni kubwa ndio maana hatutaki kusikia visingizio visivyo vya msingi katika utekekezaji wa miradi ya maji," alisema Aweso.

Aweso alisema hatakuwa kikwazo kwa viwanda atawasaidia kwa vitendo, ili waendelee kufanyakazi vizuri kwa kuzingatia ubora unaotakiwa na kwa gharama nafuu.

Alisema Wizara ya Maji inafanya mageuzi makubwa katika kuhakikisha maji yanapatikana na kuagiza wenye viwanda kuwasiliana na viongozi wake badala ya kuwatumia vishoka.

Aidha, alisema kuna changamoto katika upatikanaji wa pampu mradi unapokuwa uekamilika jambo linaloshangaza.

"Tutaanza kuchukua hatua haiwezekani mradi wa maji umekamilika alafu wanasuburia pampu kwa muda mrefu jambo hili siwezi kulikubali," alisema Aweso.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Othman Masoud, simamia mazuri ya Maalim

OTHMAN Masoud Othman Sharif, amerithi nafasi aliyoiacha Hayati Maalim Seif Sharif Hamad ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, juzi alimteua Masoud kuijaza nafasi hiyo, kufuatia kifo cha Maalim Seif kilichotokea Februari 17, mwaka huu, na jana alimwapisha katika Ikulu ya Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, ilisema kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 9(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kinachosema kwamba "Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja na lengo la kufikia demokrasia."

Ilieleza kwamba kwa mujibu wa uwezo aliopewa chini ya kifungu namba 39(3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, amefanya uteuzi huo baada ya kushauriana na Chama cha ACT-Wazalendo.

Tunampongeza Masoud kwa uteuzi huo, huku tukiamini uzoefu wake katika utumishi wa umma na usomi wake katika taaluma ya sheria vitamwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Kwa kuwa si mgeni katika utumishi wa umma kama kiongozi, ikiwamo kushika nafasi ya mwanasheria mkuu wa Zanzibar, bila shaka ataimudu nafasi hiyo, pengine ndiyo sababu iliyomshawishi Rais Mwinyi kumteua baada ya mashauriano na ACT-Wazalendo.

Chama hicho kabla ya kushauriana na Rais Mwinyi bila shaka kitakuwa kimefanya uchambuzi na tathmini ya kina ya wanachama wake kisha kumuona Masoud kuwa na sifa zote za kuijaza nafasi ya Maalim Seif.

Kauli za watu mbalimbali waliomzungumzia Masoud baada ya uteuzi huo zinadhihirisha kwamba uteuzi wake hauna shaka yoyote, hivyo kilichobakia kwake ni kushirikiana na Rais Mwinyi kuwatumikia Wazanzibari, kwa kutanguliza mbele maslahi mapana ya Zanzibar.

Mambo makubwa ambayo mtangulizi wake (Maalim Seif) aliyapa kipaumbele na kuyasimamia ni Umoja wa Kitaifa na maridhiano miongoni mwa Wazanzibari. Hayo ndiyo mambo yaliyowezesha kufanyika marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuruhusu kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) mwaka 2010.

Maalim Seif, kila mara hakusita kuhubiri amani, umoja na maridhiano kwa Wazanzibari. Hivyo ni matarajio ya wengi kwamba Masoud atafuata nyayo hizo. Pia alikuwa na ndoto za kuiona Zanzibar inapaa kiuchumi na wananchi wake wananufaika kwa kutumia rasilimali zake kama zao la karafuu, bandari na rasilimali za bahari.


Hata wakati wa kampeni zake za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 alilizungumzia kwa msisitizo mkubwa suala hili, na hata baada ya kuapishwa na Rais Mwinyi, aliahidi kuwa watashirikiana katika kupaisha uchumi wa Zanzibar hususan kupitia bahari kuu (uchumi wa bluu).

Rais Mwinyi naye suala la uchumi wa bluu ni kipaumbele chake katika kupaisha uchumi wa Zanzibari na kubadili maisha ya wananchi wake.

Kauli ya Masoud wakati wa kiapa jana ya kuahidi kushirikiana na Rais Mwinyi kuleta maendeleo na kulinda maridhiano inatia matumaini. Tunamtakia kila la kheri, tukiamini atayasimamia mambo yote mazuri aliyoyasimamia Maalim Seif.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ni muhimu kusoma mita kulipa maji kielektroniki

Na Frank Monyo

HIVI karibuni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ilianza kutoa elimu ya kusoma mita na namna ya kulipia ankara kielektroniki kwa wateja wake.

Ni hatua muhimu kwa vile kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wateja kuhusu ankara za maji kuwa kubwa ikilinganishwa na matumizi yao halisi.

Licha ya kwamba malalamiko hayo yanatokana na baadhi ya wateja kutofahamu ama kupuuza matumizi sahihi ya huduma hiyo.

Elimu hiyo iliyotolewa, inakuja wakati ambao DAWASA imesambaza majisafi na salama kwa wateja wengi wa Dar es Salaam na maeneo jirani ya mkoa wa Pwani.

Ndiyo maana ni wakati wa wateja wa DAWASA kufungua mageti ya nyumba zao wanapotembelewa na maofisa wa mamlaka hiyo, kwani elimu wanayoitoa imejikita katika kuwaelimisha kuhusu matumizi sahihi ya maji, jinsi ya kusoma mita na kuwafahamisha gharama za maji wanazopaswa kulipia kwa uniti kielektroniki.

Maji ni muhimu kwa matumizi ya binadamu tena kuna msemo kuwa maji usipoyaoga utayanywa hii inaonyesha ni kwa jinsi gani ni muhimu katika maisha ya kila siku.

Hata hivyo, wateja wengi wameshindwa kuwa wastaarabu linapokuja suala la matumizi sahihi ya maji na kwa umakini.

Familia nyingi zinahangaika kutokana na kukosekana kwa vyombo vya kuhifadhia maji kama matangi, ndoo, madumu na mapipa na hii inatoa taswira ya kukosekana umakini wa matumizi ya maji kwani kwa kuvikosa vitu hivyo ni wazi hutofahamu matumizi sahihi ya maji kwa mwezi.

Mei, mwaka jana, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kwa kuliona hili, alitoa maagizo kwa mamlaka za maji nchini kutoa elimu ya kusoma mita ili kupunguza malalamiko.

"Asilimia kubwa ya wateja hawajui namna mita zinavyohesabu, kuzisoma na gharama za kila uniti, hivyo basi ni jukumu la mamlaka kuwapa elimu hiyo kila wanapokwenda kuzisoma kwenye nyumba za wateja, naamini hatua hii itapunguza malalamiko na itaamsha ari ya kulipia huduma kwa wakati," alisema Aweso.

> **Asilimia kubwa ya wateja hawajui namna mita zinavyohesabu, kuzisoma na gharama za kila uniti, hivyo basi ni jukumu la mamlaka kuwapa elimu hiyo kila wanapokwenda kuzisoma kwenye nyumba za wateja, naamini hatua hii itapunguza malalamiko na itaamsha ari ya kulipia huduma kwa wakati," alisema Aweso.**

Ni ukweli kuwa suala la kulipia maji na hata kwenye kuhifadhi na kuyatunza ni mambo ambayo watu hawayazingatii ndiyo maana ukapita mtaani ukakuta bomba la maji linavuja nje ya nyumba, lakini wenyewe hawajali.

Unajiuliza hivi, mwenye bomba haoni maji yanapotea? Sasa ujiulize mteja kama huyu atakubali kulipa ankra ya maji ambayo ameyatumia bila utaratibu? Kwa maana hiyo DAWASA bado wana kazi kubwa ya kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya maji.

Changamoto kubwa ni jamii kutokuwa na utaratibu bora wa matumizi ya maji, kwani baadhi uacha maji yakimwagika kwenye bomba na hata wakati mwingine kuelekeza mpira wa maji kwenye bustani zao.

Hapa, ipo haja ya wasaidizi wa nyumbani na watoto kupewa elimu sambamba na kukanywa kuchezea maji, kwani wapo wanaofua ama kuosha vyombo kwenye bomba la maji bila kuteka kwenye chombo.

Lakini elimu lazima iende sambamba na umuhimu wa kulipa ankara za maji kwani kwa kufanya hivyo kutaiwezesha mamlaka kuendesha miradi mbalimbali na kuimarisha upatikanaji wa maji kwa usawa.

Mapema mwezi uliopita, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maji inayoendeshwa na DAWASA, alieleza kufurahishwa na kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na DAWASA ya usimamizi wa miradi hiyo.

Alisema anaamini ifikapo 2025 upatikanaji wa maji Dar es Salaam utakuwa ni kwa asilimia 100, huku akionyesha nia ya kuwapa DAWASA miradi ya maji nje ya Dar es Salaam kutokana na kufanikiwa katika utendaji.

Kwa maana hiyo mamlaka hiyo inayo kazi kubwa ya kufanya hasa kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya maji na ulipaji ankara kwa wakati ili miradi hiyo iwe endelevu.

HABARI KITAIFA

# TANESCO yakunwa kasi ujenzi Bwawa la Nyerere

**Joseph Mwendapole, MOROGORO**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limeelezea kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Megawati 2,115 katika Bwawa la Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) Rufiji huku mkandarasi akiahidi kukamilika Juni, mwakani.

Meneja Uhusiano wa TANESCO, Johari Kaachwamba, alisema hayo wakati wa ziara ya wahariri na waandishi wa habari waandamizi waliotembelea ujenzi wa mradi huo kujionea maendeleo yake na kuonyeshwa maeneo mbalimbali na shughuli zinavyoendelea.

Kaachwamba alisema lengo ni kuwapa wahariri uelewa mpana na kutoa taarifa sahihi kwa umma kuhusu mradi huo ambao utaliwezesha taifa kuwa na umeme wa kutosha na hata kuuza kwa nchi jirani.

Alisema shirika hilo kwa sasa linaendelea kutekeleza miradi mbalimbali mikubwa ya umeme hivyo wameona wahariri na waandishi wa habari ni nguzo muhimu ya kufikisha taarifa sahihi kwa umma. Kaachwamba alisema ni matumaini ya TANESCO baada ya wahariri kupata nafasi ya kutembelea mradi huo na kuona kila kinachoendelea, ile haki ya mwananchi kupata taarifa sahihi inakwenda kutekelezeka.

Mhandisi Mkazi wa Mradi huo, Lutenganya Kamugenyi, alisema hatua inayoendelea sasa ni kujenga ukuta wa zege utakaokamilika Oktoba mwaka huu ili kuanza kuvuna maji yatakayotumika kuzalisha umeme.

Alisema tahadhari za majanga yanayoweza kukwamisha kuendelea kwa ujenzi kama mvua zimeshachukuliwa na hata kama itanyesha ujenzi utakuwa unaendelea kama kawaida kwani maji ya mto yalishachepushwa kwenye njia zingine.

SANTANA INVESTMENT LTD

## SANTANA INVESTMENT LIMITED

Off Shekilango road, Sinza Kwaremi Muungano street, Plot B No. 335
P.O. Box 19944 DSM, E-mail: santanainvestment@yahoo.com Tel; +255787715057 +255713320653
Court Broker, Process server, Debt Collector, Tax Matters, Levies and Auction Mart
Reg Na. 114856 TIN Na. 126-205-929

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **BENKI YA NBC,** SISI KAMPUNI YA MADALALI WA MAHAKAMA YA SANTANA INVESTMENT LTD, TUTAUZA MALI/DHAMANA KWA NJIA YA MNADA KAMA IFUATAVYO:-

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO YA DHAMANA | TAREHE | MUDA | DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | YAGESA MAKUNGWI NGOMA | NYUMBA | CT.NO. 26826,L.O NO 200840, PLOT.NO.21, BLOCK 'A' HD DIDIA TRADING CENTRE, SHINYANGA I.N.O YAGESA MAKUNGWI NGOMA | 10-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | DIDIA - SHINYANGA |
| 2 | HAMIS KOMBO | NYUMBA | CT.NO. 35430-LR MWANZA, L.O NO. 423417, PLOT.NO. 36, BLOCK 'GG' SERVICE INDUSTRY,KITANGIRI AREA, SHINYANGA MUNICIPALITY I.N.OMAHONA | 10-03-21 | Saa 08:00 Mchana na kuendelea | KITANGIRI - SHINYANGA |
| 3 | SILAMU MABUGA GANHA | NYUMBA | CT NO 11523, PLOT NO.65 BLOCK JJ NDEMBEZI SHINYANGA MUNICIPALITY I.N.O GERASE BALIMUJURA RUKUMBERWA | 12-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | NDEMBEZI-SHINYANGA |
| 4 | SILAMU M. GANHA | NYUMBA | CT NO 20479 LO NO 198330 PLOT NO 3 BLOCK T MAJENGO SHINYANGAIN THE NAME OF SITTA SALU KISINZA | 12-03-21 | Saa 08:00 Mchana na kuendelea | MAJENGO SHINYANGA |
| 5 | CHARLES MAIGE MAHUSHI | NYUMBA | CT NO.224888-LR MWANZA, L.O. NO.198481, PLOT NO.609 BLOCK 'HH' (HIGH DENSITY) NDOLA AREA I.N.O MBOJE NGASSA. | 16-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | NDOLA AREA-SHINYANGA |
| 6 | NYAMALUDA BUZA MLEKANA. Co. LTD | NYUMBA | CT NO.42559-LR MWANZA, L.O. NO.195705, PLOT NO.8 BLOCK 'A' (HD) SIMA AREA, BARIADI URBAN AREA.I.N.O | 19-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | BARIADI - SIMIYU |
| 7 | MASHAKA SENGO NYANDU | NYUMBA | CT NO.36584-LR MWANZA, L.O NO.223800, PLOT NO.50 BLOCK 'B' MWAKIPUGILA, AREA, MEATU DISTRICT I.N.O MASHAKA SENGO NYANDU. | 23-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | MWAKIPUGILA AREA, MEATU, SIMIYU |
| 8 | FRIDA FURNITURE | NYUMBA | C.T NO. 20703 LR MWANZA L.O NO. 156243 PLOT NO. 320 BLOCK 'V' I.N.O JUVENALI SHABANI SHILYANGA, REGISTERED TO COVER AN UNSPECIFIED | 26-03-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | NZEGA-TABORA |
| 9 | TWAHIRU HAMISI SEMTINDI | NYUMBA | C.T.NO.23363-LR MOSHI, L.O. NO. 171445, PLOT .NO. 1116, LUKOZI AREA, LUSHOTO DISTRICT I.N.O SHAURI ATHUMANI SEMTINDI. | 09-04-21 | Saa 04:00 Asubuhi na kuendelea | LUKOZI TANGA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi anatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki cha 75% kilipwe ndani ya siku 14 toka tarehe ya kufanyika mnada, kinyume cha hapo kiasi kilicholipwa awali hakitarudishwa na mnada kufanyika upya.
2. Ukaguzi wa dhamana (nyumba au gari) utafanyika toka siku ya tangazo hili na gharama za ukaguzi na kuona dhamana hiyo ni za mteja mwenyewe.
3. Gharama za kubadili umiliki (transfer) ni za mteja mwenyewe.
4. Mnada utafanyika mahala dhamana zilipo.
5. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa Santana Investment Ltd.

**Kwa mawasiliano mengine tafadhali piga namba zifuatazo:**
**0713-320653, 0715-655950, 0767-531622, 0782-375475**

TRA

## MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA**

## TAARIFA KWA UMMA

## UWASILISHAJI WA NYARAKA ZA ULIPAJI KODI KWA MAGARI YALIYOORODHESHWA HAPA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwafahamisha wamiliki wa magari yaliyoorodheshwa katika tangazo hili kuwasilisha nyaraka zinazothibitisha ulipaji wa kodi ya uingizwaji wa magari hayo nchini.

Nyaraka hizo ziwasilishwe katika ofisi ya forodha iliyoko karibu au katika ofisi ya Kanda ya Upelelezi wa Kodi katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kujiridhisha.

Wito huu ni kwa mujibu wa kifungu Na. 235 cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004.

Wahusika wanahimizwa kuwasilisha nyaraka hizo ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kwanza ambayo tangazo hili limetolewa ambayo ni tarehe 3 mwezi wa Machi 2021.

Endapo mhusika yeyote hatatoa ushirkiano, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi zingine za Serikali italazimika kukamata na kutaifisha gari husika kwa mujibu wa kifungu Na. 200d (iii) cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na**

**KAMISHNA WA UPELELEZI WA KODI**

**EAGT MOTOR VEHICLES**

| S/N | Reg. Number | Make | Chassis |
|---|---|---|---|
| 1 | T556 BGT | NISSAN ATLAS | G4H41001784 |
| 2 | T931 AKN | NISSAN ATLAS | G4H41001237 |
| 3 | T544 BXT | MITSUBISHI DION | CR6W0103808 |
| 4 | T501 BMY | VW BORA | WVWZZZIJZW4702884 |
| 5 | T504 BMY | VW PASSAT | WVWZZZ3BZWE320448 |
| 6 | T475 BTJ | TOYOTA GARIB | AE1147015605 |
| 7 | T926 BBH | TOYOTA RAV4 | JTEHH20V700127049 |
| 8 | T919 DFG | TOYOTA PRADO | VZJ950005517 |
| 9 | T464 DFT | TOYOTA CANDER | RZJ950034921 |
| 10 | T688 DGF | TOYOTA L/CRUISER | UZJ1000138418 |
| 11 | T959 DGK | TOYOTA NADIA | SXN150006052 |
| 12 | T386 BDS | TOYOTA MARK2 | GX1006162093 |
| 13 | T999 BWC | TOYOTA NOAH | SR400210254 |
| 14 | T184 CDY | NISSAN SERENA | TC24331168 |
| 15 | T467 ATS | SUZUKI ESCUDO | TDIIW100883 |
| 16 | T787 CEK | SUZUKI CARRY | DD51T370806 |
| 17 | T531 ANF | HONDA | L125S5418745 |
| 18 | T990 AJX | MITSUBISHI | JMBLNN38WR2300118 |
| 19 | T602 AVE | PEUGEOT | VE355181703167149 |
| 20 | T210 AVY | TOYOTA L/CRUISER | FZJ800026512 |
| 21 | T194 BXQ | TOYOTA LITEACE | MD2DDDMZZUWG75551 |
| 22 | T212 DCJ | TOYOTA COASTER | H2B500009960 |
| 23 | T577 CCL | TOYOTA RAV4 | SXA117026088 |
| 24 | T629 CDT | SUNLG | LY4YBCJC3CK000478 |
| 25 | T218 BPS | SKYMARK | B2INEF08K10X00027 |
| 26 | T798 DAG | SANLG | LBRSPJB51E9017570 |
| 27 | MC356 ARE | KING LION | LTBPK8BG3E2K10425 |

# Lukuvi ageukia vijiji vinavyoibukia miji

**Na Munir Shemweta, MAGU**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezitaka wilaya zote kutambua maeneo yote ya vijiji yanayochipukia kuwa miji na kuyapangia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Lukuvi alisema hayo jana wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Mwanza.

Alisema baada ya serikali kuweka jitihada kubwa katika kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), sasa vijiji vinaishi kimji na maisha yamebadilika na vingi vimekuwa miji.

Kutokana na hali hiyo, alisema ni vizuri halmashauri ambazo ni mamlaka ya upangaji kuangalia ni vijiji gani vimechipukia kimji na kuvipangia matumizi bora ya ardhi yatakayoainisha shughuli kama vile kilimo, ufugaji na kusisitiza kuwa wasipofanya upangaji mapema watashindwa kuvipanga baadaye.

Lukuvi alisema katika maeneo ambayo vijiji havina sifa ya kuchipukia kuwa miji, halmashauri zisimamie ujenzi wa makazi kwa kuviwekea utaratibu wa kujenga nyumba kwa mpangilio ulio bora.

"Kazi ya kupanga vijiji ni ya halmashauri. Kama ambavyo mnapanga kujenga madarasa matano kwa mwaka katika halmashauri, basi muweke malengo ya kupanga vijiji 10 kwa mwaka," alisema Lukuvi.

Katika hatua nyingine, Waziri Lukuvi alikagua mradi wa upimaji ardhi eneo la Kisesa katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu na kuitaka halmashauri hiyo kuwatumia watendaji wa serikali katika kazi ya upimaji badala ya kutegemea kampuni za upimaji alizozielezea kuwa wakati mwingine zimekuwa zikiwatoza fedha nyingi wananchi.

"Tumieni watumishi walio katika halmashauri kushambulia kupima maeneo mbalimbali na vifaa vya upimaji vipo vya kutosha katika ofisi za ardhi za mikoa," alisema Lukuvi.

Pia alisema kama halmashauri zitashindwa kupima maeneo kutokana na uchache wa watumishi, zichukue wanafunzi wa vyuo vya ardhi. Aliagiza kazi zote zilizoshindwa kufanywa na kampuni za upimaji, sasa zifanywe na watendaji wa sekta ya ardhi wa serikali.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Eliah Kamyanda, alisema Mwanza ni moja ya mikoa 16 iliyopewa fedha na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya programu ya kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema programu hiyo inatekelezwa katika maeneo ya Kisesa na Bujora na wanatarajia kupima viwanja 3,000.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati), akikagua mabomba ya maji yanayotengenezwa na Kiwanda cha Tanzania Steel Pipes Ltd (TSP) wakati wa ziara yake, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makore na Mkuu wa Udhibiti Ubora wa Kiwanda cha TSP, Festo Temba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aanzisha kampeni maalum kumaliza ukosefu wa mabweni

**NA Frank Kaundula, MOROGORO**

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, ameanzisha kampeni maalumu ya ujenzi wa mabweni kwa shule zote za sekondari ili ifikapo mwakani kusiwe na mwanafunzi yeyote atakayekuwa akisoma huku akikaa nyumbani kwa wazazi.

Ole Sanare aliyasema hayo juzi wilayani Malinyi wakati akizungumza na wanafunzi, walimu, viongozi mbalimbali wa serikali na wakazi wa wilaya hiyo kwenye hafla ya kuwapongeza wanafunzi wa shule za msingi wilayani humo.

"Kuna changamoto ya wanafunzi wengi kutembea umbali mrefu kwenda shuleni hali ambayo imekuwa ikichangia watoto kushindwa kuwahi vipindi darasani ikiwa ni pamoja na suala la utoro, hivyo mabweni yatatatua changamoto hii," alisema Sanare.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, mkoa umeamua kuanzisha kampeni ya ujenzi wa mabweni ambayo yatatumiwa na wanafunzi hasa wale wanaoishi kwa kupanga kutokana na baadhi ya shule kuwa mbali.

Mkuu wa mkoa alisema kitendo cha wanafunzi kuishi kwenye mabweni, kitasaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika shule zote za mkoa, hivyo kusaidia kukuza taaluma kwa watoto, shule na pia kuleta heshima kubwa kwa mkoa.

Sanare aliipongeza Wilaya ya Malinyi kwa kufanya vizuri mitihani ya taifa ya kuhitimu elimu ya darasa la saba mwaka jana. Alisema kitendo hicho kiliwafanya walimu wa shule hizo kutembea kifua mbele.

Mkoa wa Morogoro ulishika nafasi ya nane katika matokeo ya mtihani wa taifa darasa la saba mwaka jana na Malinyi ilishika nafasi ya kwanza kati ya halmashauri zote tisa za mkoa huku ikifikisha ufaulu wa asilimia 96.

Wilaya hiyo ilishika nafasi ya tisa kitaifa katika matokeo ya mitihani wa darasa la saba mwaka jana licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo upungufu wa walimu.

Nao wanafunzi walipongeza mpango huo wa ujenzi wa mabweni, huku wakisema utasaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kutembea umbali mrefu kutoka maeneo ya makazi hadi ziliko shule walizochaguliwa. Mbunge wa Malinyi, Antipas Mgungus, alisema atakuwa mstari wa mbele kutekeleza mpango huo wa kujenga mabweni katika shule zote za serikali ili kutatua tatizo la kutembea umbali mrefu.

# DC ataja suluhu uhaba madawati

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Mhandisi Martine Ntemo, amewataka walimu kufanyia ukarabati madawati yanayoharibika kwenye shule zao kuepuka upungufu ambao unaweza kutokea.

Ntemo alitoa agizo hilo jana mjini hapa alipokuwa akizungumza na walimu na wanafunzi wa Shule za Msingi za Maendeleo na Maili Moja wakati wa kukabidhi madawati 250 yaliyotolewa na Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Ntemo alisema serikali inaendelea na mpango wa kukabiliana na kero za sekta ya elimu ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma kwenye mazingira rafiki yatakayoinua kiwango cha ufaulu.

Aliipongeza halmashauri kwa kutoa madawati hayo ambayo yatasaidia kukabili tatizo la baadhi ya wanafunzi kukaa chini ambapo aliwataka kuhakikisha wanafanya ukarabati pale madawati yanapoharibika.

Mkuu wa Wilaya aliwaomba wadau wa elimu kuendelea kuchangia sekta hiyo ili kupunguza kero zilizopo kwenye sekta hiyo ambayo inaandaa wanafunzi ili kuja kuwa viongozi bora wa baadaye.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Jennifer Omolo, alisema halmashauri kwa sasa ina upungufu wa madawati 2,000 kwa shule za msingi na kwenye karakana ya Iramba, wametengeneza madawati 500 na karakana ya Mtaji wa Maskini ni Nguvu Zake Mwenyewe, wanatengeneza madawati 200 ambayo yatapunguza uhaba uliopo.

Alisema madawati yaliyosalia watayatengeneza kabla ya Julai, mwaka huu, kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayekaa chini.

Omolo alisema wiki mbili zijazo watakabidhi madawati kwa shule zingine na watahakikisha madawati mabovu wanayakarabati ili kupunguza tatizo hilo kwenye shule za halmashauri hiyo.

**Aliipongeza halmashauri kwa kutoa madawati hayo ambayo yatasaidia kukabili tatizo la baadhi ya wanafunzi kukaa chini ambapo aliwataka kuhakikisha wanafanya ukarabati pale madawati yanapoharibika.**

HABARI KITAIFA

## WMA yalia na vipimo sahihi kwa w'biashara

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA), umewahimiza Watanzania kutumia vipimo sahihi na kuwafichua watu wasiowaaminifu na wafanyabiashara ambao wamekuwa wakitumia vipimo batili kuwapunja walaji.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja Uhusiano wa WMA, Irene John, wakati wa wiki ya viwanda kwa wanawake wafanyabiashara na maonyesho ya bidhaa mbalimbali.

Alisema wakati nchi ikiingia kwenye uchumi wakati, ni vyema wafanyabiashara wakazingatia umuhimu wa kutumia vipimo sahihi ili kuhakikisha walaji hawapunjwi kwa bidhaa wanazonunua.

"Lengo la WMA kuja hapa ni kuwaelimisha wajasiriamali wadogo umuhimu wa vipimo sahihi ili watoke kwenye udogo ili wakue na kufikia wafanyabiashara wakati na wakubwa."

Alisema serikali imefungua masoko mbalimbali ya madini na wakala wa vipimo umekuwa ukifanya ukaguzi wa vipimo vinavyopimia madini hayo

Alisema lengo la ukaguzi wa vipimo vinavyotumika ni kuwezesha wachimbaji wadogo na wakubwa wapate stahiki zao na kusiwe na ujanja ujanja wa kuwapunja.

## Walia adha usafiri kufuata matibabu

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAKAMU Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Apolinary Macheta, amesema wakazi wa Tarafa ya Kipeta wanakabiriwa na adha kubwa ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya kutokana na tarafa hiyo kutokuwa na kituo cha afya.

Aliyasema hayo alipokuwa katika Kijiji cha Tululu wilayani Sumbawanga wakati akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, katika mkutano wa hadhara na wanakijiji.

Alisema wananchi wa tarafa hiyo bado wanapata usumbufu mkubwa na kutumia gharama kubwa kufuata huduma za afya nje ya tarafa hiyo hasa wanapohitaji huduma za upasuaji.

Macheta alisema kuwa pia zipo kata nyingi katika halmashauri hiyo hazina vituo vya afya kitendo kinachosababisha kuchelewa kupata huduma za afya kwa wakati kwa kuwa wanalazimika kuzifuata mbali.

Aliiomba serikali kuwasaidia kwa kuwajengea vituo vya afya katika tarafa yao ili kuyalinda maisha yao kwa kupata huduma za afya karibu.

# Eneo la maziko kikwazo kikubwa jiji la Mwanza

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

JIJI la Mwanza linakabiliwa na uhaba wa maeneo ya maziko katika kata mbalimbali, na kwamba yaliyopo hayatoshi na mengine yameshajaa.

Kilio hicho kilitolewa jana jijini Mwanza na baadhi ya madiwani katika kikao cha Baraza la Madiwani na kutaka litengwe eneo lingine eneo la Luchelele na Kanindo ili lianze kutumika.

**Eneo la maziko limeshapatikana, na kwamba wananchi wameishalipwa fidia ili waondoke.**

Walisema kwa baadhi ya wananchi wakifiwa na ndugu zao wanapata shida sehemu za kuzika, na kwamba umefika wakati eneo lililoandaliwa na Jiji hilo lianze kutumika.

Diwani wa Isamilo, Charles Nyamasiriri, alisema, wananchi wanakabiliwa na tatizo hilo, na kwamba imefikia hatua kaburi linachimbwa juu ya kaburi lingine.

Diwani wa Mandu ambaye ni Meya wa Jiji la Mwanza, Sima Constantine, aliunga mkono hoja hiyo, na kwamba umefika wakati wa kupata eneo kubwa kwa ajili ya maziko.

Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, alisema eneo la maziko limeshapatikana, na kwamba wananchi wameishalipwa fidia ili waondoke.

Aliwataka wananchi waliolipwa fidia kuhama haraka na kuachia eneo hilo, ili taratibu zingine zifanyike na watu waanze kuzika ndugu zao huko.



Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi, Edmund Massawe, akizungumza katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja cha mjini Liwale juzi na kuhimiza vyama hivyo mkoani humo kufanya mikutano kwa wakati kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha wa 2021/ 2022. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jamii yaaswa kutonyanyapaa wenye VVU

**Na Enock Charles**

WATANZANIA wametakiwa kuacha unyanyapaa kwa watu wenye Virusi vya Ukimwi (VVU) ili kuwawezesha kuishi maisha marefu kama watu wengine.

Imeelezwa kuwa bado upo unyanyapaa kwa watu wenye virusi hivyo katika jamii ya Watanzania.

Akizungumza katika siku ya kupinga unyanyapaa kwa wenye VVU yenye kauli mbiu ya "Tokemeza unyanyapaa na ubaguzi, timiza haki sawa kwa wote", Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga, amewaomba wananchi kuwathamini watu wenye wanaoishi na VVU na kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za kijamii.

"Unyanyapaa mara nyingine unaleta sonona kwa watu wenye maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na kushindwa kushiriki shughuli za kijamii, kwa hiyo nitoe rai kwa wanajamii wote kuendelea kuwathamini na kuwashirikisha kikamilifu ili wajione ni watu sawa na watu wengine," alisema Ummy.

Alisema ni muhimu kwa jamii kukabiliana na vikwazo ambavyo vinaiweka katika hatari ya maambukizi ya VVU kwa kubadili tabia na mienendo kuanzia katika jamii, familia na mtu mmoja mmoja ikiwamo kuendelea kutumia dhana za kujikinga na virusi hivyo ili kupunguza athari za ugonjwa huo katika kampeni ya 90 90 90 na pia kupunguza ubaguzi kufikia asilimia 0 ifikapo mwaka 2030.

Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, Samueli William, alisema ubaguzi kwa waathirika wa VVU unaongeza madhara kwa waathirika hao na kukwamisha mpango wa umoja huo kumaliza tatizo la Ukimwi duniani ifikapo mwaka 2030.

Alisema maambukizi kwa watu wazima na vijana kuanzia miaka 15-49 yamepungua kutoka asilimia 5.1 hadi 4.8 katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, lakini kiwango cha maambukizi kwa wanawake ni kikubwa kuliko kwa wanaume kwa asilimia 6.2 na kwamba ili kufikia malengo ya Umoja wa Mataifa kumaliza tatizo la Ukimwi ni muhimu pakawepo ushirikiano kutoka kwa wadau wote, serikali na jamii.

HABARI KITAIFA

# Miradi aliyozindua JPM yawakosha Dar

**Na Anaeli Mbise**

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wamefurahishwa na hatua ya Rais John Magufuli, kuzindua miradi ya mbalimbali ndani ya mkoa huo hivi karibuni.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao walisema kuwa miradi hiyo itachochea kukuza fursa za kiuchumi pamoja na maendeleo ya kijamii.

Mhandisi Mtendaji wa kampuni ya ujenzi ya Tanzania Building Works, Mohamed Noray, alisema miradi ya maendeleo inayojengwa ndani ya Dar es Salaam, itasaidia katika kukuza siyo tu pato la mtu mmoja mmoja bali pia uchumi wa mkoa utakua zaidi.

**Baada ya miundombinu kuboreshwa kwenye soko letu la Kisutu sasa matumaini yetu wateja wataongezeka kwa kasi kubwa...**

"Rais wetu amefaulu sana katika miradi ya mioundombinu hasa barabara kwa mfano, hapa daraja la Kijazi Ubungo kulikuwa na foleni ambayo inachelewesha watu kufika kwa haraka sehemu za katikati ya jiji, ila sasa panafikika kwa urahisi na itazidi kuokoa uchumi wa mkoa, maana muda mwingi ulikuwa unapotea kwenye foleni hizi," alisema Noray.

Aron Kimaro, mkazi wa Kimara Suka katika Manispaa ya Ubungo, alisema ujenzi wa daraja la Kijazi Interchange umemsaidia kufika ofisini kwake kwa wakati na pia kukuza kipato cha biashara ambazo anazifanyia Kariakoo.

"Kiukweli zamani tulikuwa tunatoka asubuhi sana nyumbani kama saa kumi na moja ili kuwahi foleni ya Ubungo, lakini tangu kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Ubungo unaweza kutoka hata saa moja asubuhi na kufika ndani ya dakika 40 tu hii ni hatua nzuri kwetu ambao tunaitumia hii barabara ya Morogoro," alisema Kimaro.

Kimaro aliongeza kuwa fursa nyingine ambayo imepatikana kutokana na ujenzi wa daraja hilo ni pamoja na ajira ambazo zimekuwa zinapatikana kwa vijana, jambo ambalo limesaidia kupunguza tatizo la ajira kwa wakazi wa Ubungo na mkoa kwa ujumla.

Ashura Athumani, mfanyabiashara wa nafaka katika soko la Kisutu, alisema ujenzi wa soko la kisasa litawasaidia kupata wateja wengi zaidi.

"Baada ya miundombinu kuboreshwa kwenye soko letu la Kisutu sasa matumaini yetu wateja wataongezeka kwa kasi kubwa, maana lilivyokuwa awali lilikuwa na mandhari ambayo haihiridhishi sana nampongeza sana Rais wetu Magufuli," alisema Ashura.

Wiki iliyopita, Rais Magufuli alifanya ziara ya siku tatu mkoani Dar es Salaam, na alizindua miradi ya daraja la Kijazi Interchange, majengo ya chuo cha polisi Kurasini, kuzindua jengo la Jitegemee, stendi ya mabasi ya Magufuli Bus Terminal Mbezi Luis, na aliweka jiwe la msingi katika soko la Kisutu.




Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya Tanzania Building Works, Mhandisi Mohamed Noray, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, alipotembelea mradi wa daraja la juu la Kijazi (Kijazi Interchange), katika makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela, eneo la Ubungo, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: ANAELI MBISE**

# Viwanda vya mabomba ya maji kusaidiwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amevihakikishia viwanda vya kutengeneza na kusambaza mabomba ya maji kutatua matatizo yanayowakabili ikiwamo uvamizi wa bidhaa feki sokoni.

Pia ameitaka Wizara ya Maji kuhakikisha inaendeleza uhusiano mzuri na wadau wa sekta ya maji kwa kushirikiana pamoja.

Aliyasema hayo juzi alipofanya ziara mkoani Dar es Salaam katika kampuni ya kuzalisha mabomba ya PLASCO LTD ambapo pamoja na mambo mengine, aliitaka kuongeza uzalishaji wa mabomba yenye viwango bora na usambazaji, kwa sababu kuna miradi mingi ya maji inayohitajika kukamilika.

Aweso alisema: "Onyesheni hiyo teknolojia yenu mpya ya kutengeneza mabomba ya Weholite hasa katika maadhimisho ya Wiki ya Maji mwezi huu. Anzisheni miradi ya maonyesho katika maeneo mbalimbali. Mkiionyesha wataalamu wetu wataiona na watasaidia kuisambaza katika maeneo mengi nchini."

Waziri Aweso alisema kilio kikubwa cha makandarasi wengi nchini wa miradi ya maji ni ukosefu wa mabomba kwamba hayapatikani kwa wakati, kumbe kuna kampuni kadhaa zinazozalisha mabomba mengi na yenye viwango ikiwamo PLASCO.

"Kuanzia sasa sitaki kusikia mkandarasi akisingizia ukosefu wa mabomba, kwamba ndiyo unamkwamisha kukamilisha miradi, kwa sababu kuna kampuni nyingi za kuzalisha mabomba hayo na yenye ubora," alisema Aweso.

Alisema kama kuna mkandarasi ataendelea kusingizia ukosefu wa mabomba, ataondolewa, na kwamba wizara itatumia wataalamu wake kukamilisha mradi huo.

Alisema hatua ya wizara kutumia wataalamu wake kutekeleza miradi ya maji imeokoa fedha nyingi na kufanikiwa kutekeleza miradi 192 iliyokwama.

Alisema miradi hiyo endapo ingeendelea kutekelezwa na makandarasi waliojaa visingizio visivyokwisha, ingegharimu Sh. bilioni 207, lakini kwa kutumia wataalamu wa wizara imetumia Sh. bilioni 193.

Ofisa Uendeshaji wa Kampuni ya PLASCO LTD, Alimiya Osman, alisema wanafurahi kutembelewa na Waziri wa Maji na uongozi Wakala na Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), akiahidi kushirikana nazo zaidi.

Alisema wanazalisha malighafi za tani 28,000 kwa mwaka na katika tani hizo asilimia 70 ni mabomba ya HDPE.

# Mrajisi awatia moyo wakulima wa korosho

**Na Sabato Kasika,** LIWALE

MRAJISI Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Lindi, Edmund Massawe, amewataka wakulima wa korosho kutokata tamaa baada ya kushuka kwa uzalishaji wa zao hilo msimu uliopita, badala yake iwe ni fursa kwao kujipanga upya kwa ajili ya msimu ujao.

Aidha, amewataka wasitafute 'mchawi', bali watambue kuwa uzalishaji wa mazao una matatizo ambayo wakati mwingine yapo ndani ya uwezo wao au juu ya uwezo wao.

Alitoa maelekezo hayo juzi, katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja cha mjini Liwale, baada ya kusomwa kwa taarifa ya Umoja ya msimu uliopita ambayo ilionyesha kushuka kwa uzalishaji wa zao hilo.

Taarifa hiyo ilisomwa na mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako, ikionyesha kuwa Umoja kilitarajia kukusanya tani 3,300 katika msimu wa 2020/2021, lakini makusanyo yalishuka hadi tani 1,700.

Alisema, kushuka kwa uzalishaji kunaweza kuwa kumechangiwa na sababu nyingi, zikiwamo ambazo ziko ndani ya uwezo wa wakulima, na kwamba kuzitatua, na zile za kitaalamu, waachiwe wataalamu wa kilimo.

Kwa upande wake Mpako, aliwataka kujadili na kutoa ushauri wa jinsi gani wanaweza kurudisha hali ya uzalishaji na kukusanya korosho nyingi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mpako pia alisema, kuna haja ya kupitia na kuwachambua wanachama ambao hawazalishi na hawauzii mazao yao kwenye chama hicho na pia rekodi za kila mwanachama kuhusu uzalishaji wake na kumfanyia tathmini.

Polepole na mjadala wa kurefusha urais wa JPM



Ukurasa 12



Ukurasa 14

**NI OTHAM MASOUD**



UCHAMBUZI

# Kifo cha Seif kilivyozima ndoto za Profesa Lipumba

■ Aambiwa aache kumwota Hamad aangalie wengine



Profesa Ibrahimu Lipumba (kulia), akiwa na Maalimu Seif Sharif wakati wa uhai wake. Kufariki kwa Seif kumekwamisha mshikamano wa kusaka katiba na tume mpya ya uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

**Sabato Kasika**

BAADA ya kutengana kutokana na mgogoro wa kiuongozi, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, anasema alitamani kuungana na aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Shariff Hamad, ili kuanzisha mjadala na mikakati ya kudai tume huru ya uchaguzi na katiba mpya.

Chama hicho kiliingia katika mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka mitatu na kusababisha kigawanyike makundi mawili yaliyohasimiana, likiwamo la upande wa Prof. Lipumba na jingine lililokuwa linamuunga mkono Maalim Seif ambalo lilijiunga na ACT-Wazalendo na kujiengua CUF.

Mgogoro huo ulioanza mwaka 2016, ulihitimishwa Machi 2019, huku Maalim Seif na baadhi ya wanachama waliokuwa wakimuunga mkono wakihamia ACT-Wazalendo.

Kitendo cha mwanasiasa huyo kuhama CUF, kilisababisha chama hicho kupata pigo ambalo lilikifanya kikose nguvu kama kilivyokuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Wakati mgogoro wa kiungozi ukiwa umewatenganisha, mwezi uliopita, Prof. Lipumba alikaririwa na vyombo vya habari akimwomba Maalim Seif na wanachama aliohama nao kurudi kundini, ili kushirikiana kudai tume hiyo.

Ni katika hafla ya kuwakumbuka wanachama wa CUF waliopoteza maisha mwaka 2001 wakati wa maandamano ya amani, Mwenyekiti wa CUF anawaomba wanachama wote waliohama CUF kurejea katika chama na kuganga yajayo huku wakiachana na yaliyopita.

Aidha, CUF imeshasema haitashiriki katika uchaguzi mkuu hadi itakapopatikana tume huru ya uchaguzi na inatafuta kuungwa mkono katika harakati hizo za kutaka tume huru na katiba mpya.

Awali Profesa Lipumba baada ya kutangazwa matokeo ya uchuguzi mkuu wa mwaka 2020 alisema anachofanya ni kampeni za kupata katiba mpya na tume huru ya uchaguzi na maelezo hayo kuna wakati aliyatoa kwa Rais John Magufuli, akikazia zaidi suala la katiba mpya.

**WAZO LAPINGWA**

Naibu Katibu Mwenezi wa ACT- Wazalendo Taifa, Janeth Rithe, anasema chama hicho hakina muda wa kujadili maoni ya Lipumba na kwamba kinaona ni ya kawaida ambayo hayawezi kuchukuliwa kwa uzito.

"Kwanza kabisa ieleweke kuwa Maalim Seif na wenzake walifukuzwa CUF siyo kwamba walihama tu na wakaona chaama pekee ambacho wanaweza kujiunga nacho ni ACT-Wazalendo," anasema Rithe.

Rithe anaeleza kuwa Maalim Seif ameshafariki dunia, hivyo kuendelea kujadili suala la Lipumba kumtaka arudi CUF halina uzito tena na kwamba chama hicho kina mambo mengi ya kufanya.

"Mtuombee tuwe na nguvu na kujiimarisha zaidi, hayo ya Lipumba tumwachie mwenyewe, ila ni muhimu kutambua kuwa waliohama kwetu kutoka CUF, waliona kuwa huku ndiko sehemu sahihi ya kuendesha siasa," anasema akitoa maoni iwapo chama chao kitamsikiliza Lipumba au aliwasiliana nacho rasmi kujadiliana dokezo hilo.

**VYAMA KUUNGANA**

Kutokana na kifo cha Maalim Seif ambaye Prof. Lipumba alitamani arudi CUF na wenzake, Katibu Mkuu mstaafu wa TLP, Nancy Mrikaria, anasema, ni vyema sasa CUF kuungana na vyama vingine katika harakati za kudai haki na masuala ya msingi kama katiba mpya ambayo italeta tume huru ya uchaguzi.

Mrikaria anasema, kwa kufanya hivyo, hatua hiyo inaweza kusaidia, kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, bali kuendelea kudai tume huru bila vyama vya upinzani kuwa na mshikamano wa pamoja ni tatizo.

"Chama kimoja kususa uchaguzi inaweza isiwe njia ya kufanikisha lengo, kwa kuwa vingine vitashiriki kama kawaida na hivyo kile kinachosusa kuonekana hakina umuhimu wowote katika jamii," anasema Mrikaria na kusisitiza kuwa kama vyote vitaungana na kufanya maamuzi mamoja kutakuwa na matokeo chanya.

Anasema, njia bora ni Prof. Lipumba kupeleka wazo kwa viongozi wenzake wa vyama vingine na kuwashawishi waone kama watakubaliana naye ili waungane katika harakati hizo za kudai tume huru.

"Juhudi za kutaka kurejesha wanachama waliohamia CUF ili kuungana kudai haki zisiishie huko, zielekezwe kwa vyama vingine na kuvishawishi vione umuhimu huo na kumuunga mkono," anasema.

Maalim Seif ambaye Prof. Lipumba alitamani waungane tena, kwa kuwa alikuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa, hayupo, kilichobaki ni kutafuta washirika wengine kama ilivyokuwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), ulioanzishwa wakati wa bunge la katiba mpya ili kutetea kile kilichotolewa na wananchi ndani ya rasimu ya katiba.

"Kama ambavyo baadhi ya

INAENDELEA UK. 12



Humphrey Polepole. **PICHA: MTANDAO**

# Polepole na mjadala wa kurefusha urais wa JPM

## Mapambano kiitikadi yaanza bila kujieleza kiuwazi

**Na Ani Jozeni**

MBUNGE wa kuteuliwa na Katibu Mwenezi wa CCM, Humphrey Polepole, majuzi alifanya moja ya kazi anazotazamiwa kuzifanya bungeni kila inapobidi ya kuweka wazi msimamo wa chama, au hisia za uongozi katika chama hasa kwa ngazi ya Halmashauri Kuu na Kamati Kuu. Ilikuwa ni kuhusiana na suala la kurefusha urais wa Dk. John Magufuli, kwa miaka mingine mitano baada ya muhula wa pili kumalizika mwaka 2025.

Hata hivyo, jambo hilo ameshalieleza kuwa hana hamu nalo na baadhi ya wabunge wanalipigia debe ila hakuna anayejua nini hatima ya hitaji hilo kisiasa, kwani linalenga kuzua hofu ya nini kitatokea JPM akiondoka, hivyo wanamtaka abaki.

Kuna msemo wa Kiswahili kuwa 'lisemwalo lipo, kama halipo laja,' ambao una maana kuwa baadhi ya wabunge wanataka kuwe na mkakati halisi katika CCM, kuanzia bungeni wa kutaka JPM abaki, na kwa sababu ni mada imeanza kuwekwa mezani tangu muhula wa kwanza, siyo lazima ijiondoe hivi hivi tu. Wanaotoa mada hiyo wanajua utamaduni wa CCM kuhusu mihula ya urais na wanafahamu ambacho hadi leo kimezungumzwa kuhusu suala hilo, kwa mfano Rais Dk. Salmin Amour alipotaka kuendelea kukaa madarakani mwaka 2000 kwa hoja kuwa bado anapendwa, Makamu wa Rais kwa wakati ule Dk. Omar Ali Juma, alimcharukia: " Unaondoka wakati bado unapendwa, na siyo ungoje hadi uanze kupigwa mawe."

Ndicho kinachotokea pale serikali inapodumu madarakani kwa zaidi ya mihula miwili, kuwa sasa inaingia katika mandhari ya kutaka ipigwe mawe na wananchi ili iondoke ikulu na wakati huo wafuasi wake au wadau, wamejichimbia serikalini hawasikii la mtu. Ndicho kitakachotokea pale muda wa urais ukirefushwa kuwa miaka, upishane na kuchaguliwa wabunge ambako hakuna aliyewahi kutaka vipindi vyake pia virefushwe, ila muda wa urais. Wakishapishana, watasema rais aanze mihula upya, aliingia madarakani kabla ya katiba mpya kama ilivyokuwa kwa Burundi.

Ndiyo hapo linakuja suala tatanishi ambalo aliwahi kulizungumzia kiongozi wa mapinduzi ya Russia au Urusi ya zamani, Vladimir Lenin, katika insha 'nani rafiki na adui wa mapinduzi yetu?' Suala hapa ni kuwa kwa vile kuna mapinduzi yanayoendelea hapa nchini yakisimamiwa na Dk. Magufuli, hao wanaotaka aongezewe muda wa urais kwa udi na uvumba ni marafiki wa mapinduzi hayo au ni maadui zake?

Na kwa maana hiyo vile vile, wabunge walioanzisha harakati ya JPM kuongezewa muda au hata mihula, ni marafiki wa mapinduzi anaoyaendesha au ni 'waona mbali' wanaobuni mkakati rasmi wa kuyalemaza?

Kuna msemo wa injili unaosema : Si wote wanaoniita bwana, bwana watauona ufalme wa mbinguni,' na hiyo siyo wote wanaotaka JPM aongezewe muda wa uongozi wanaounga mkono kwa dhati mapinduzi yanayoendelea. Tatizo linakuja katika kupambanua kipi ni kipi, inaitwa kwa Kiswahili 'pumba na mchele' katika kampeni ya JPM kubaki madarakani, kama inaongozwa na wanaotaka jema kwa kazi anayoifanya sasa au ni wanaotaka kuididimiza, na huenda labda wamechanganyika. Ndiyo hapo kuna giza la mikakati ya siasa ndani ya CCM, ambako makundi yanajuana kwa ishara yanataka nini.

Tuanze kwa kuuliza swali, kuwa wanaotaka kinachoendelea sasa hivi kibakie hivi miaka mitano kuanzia sasa, mwelekeo wao wa kisiasa utakuwa upi, na wanaotaka kuwe na mabadiliko CCM irudi usingizini na kundi la 'walaraha' lirudi madarakani, wanaweza kufuata mipango gani? Hao wanaotaka kuendeleza urais wa JPM wanataka kurahisisha mkakati upi kati ya hiyo miwili, au kuna mkakati wa tatu ambao haupo katika upeo wa kila siku kuhusu migongano ya kiitikadi katika CCM? Migongano ya kiitikadi kimsingi inalenga maslahi ya makundi makubwa ya watu na siyo kundi dogo, hivyo makundi yenye maslahi maalum lazima yatafute kujibaraguza kwa kundi kubwa zaidi ili kuchomekeza ajenda yao mle.

Mwalimu Nyerere aliwahi kuainisha suala hilo akijadili wanaoatumia 'vipesa' kutafuta njia ya kwenda ikulu, akisema 'kabla ya kununua watu, inabidi wewe ununuliwe kwanza,' kuwa mtu hawezi kuwa na fedha nyingi zisizo na kazi azielekeze kuutafuta urais, wakati 'hakuna biashara ikulu.' Ila akipata fedha kama hizo kwa wadau ambao wanajua watazirudisha kwa njia gani akiingia madarakani, ndiyo hapo ataanza kuwanunua watu na fedha hizo, kwa sababu yeye ameshanunuliwa tayari.

Mivutano ya aina hiyo haiwezi kukosekana katika uchaguzi mkuu kokote pale, kwani serikali inaamua hatima ya maslahi yote makubwa, kwani mwelekeo wa kisera tayari ni kiama kwa maslahi ya aina moja au nyingine; kuanzia tu. Ukiangalia kwa karibu unakuta kuwa mwanasiasa au mbunge ambaye kweli anataka mapinduzi ya sasa hivi yaendelee hatang'ang'ania kuwa JPM, aongezewe muda au muhula ili ayafikishe yanakotakiwa. Ambacho angefanya ni kuangalia kama kati ya viongozi wa ngazi za juu wa sasa yuko ambaye kwa hali yoyote ile anaonekana kuwa na hamasa ya kweli ya kuendeleza kile kilichopo na kujenga mkakati wa kisiasa wa uendelezaji wake kwa upande mmoja.

Mwishowe ndiyo lingezuka suala la kuelekeza utii wa chama kwa mtu kama huyo, huku ikijulikana kuwa anatazamiwa au ana dhamira ya kufuata sera zile zile.

Ina maana shauku ya kuendeleza uongozi wa JPM ingebidi utokane siyo na ubora wa sera zinazofuatwa ila wasiwasi kuwa hapatakuwa na mtu mwenye uwezo wa kuendelea nazo, jambo ambalo si rahisi kudai kuwa tuko katika hali kama hiyo. Bado miaka 4.5 hadi kufikia kupatikana jina la mgombea wa CCM na tayari watu wameshafikia tamati kuwa hawezi kupatikana mwenye dhamira ya kuendeleza sera hizi ni kama kuna pupa ya aina fulani ambayo si njema kwa uongozi au kupima viongozi waliopo, kutoa hukumu kabla ya wakati na kuamini kuwa haiwezi kuwa vinginevyo. Uhakika huo unaficha ajenda gani?

Ndiyo hapo unaanza kuwa na wasiwasi wa uharaka wa suala hilo, na pia tatizo la kutetea hisia kama hiyo katika demokrasia. Kwa mfano ingekuwa ni kweli kuwa hatapatakiwa na kiongozi mwenye uwezo wa kuendeleza anachokifanya JPM kwa mapana yake na ikawa bayana kinadharia kuwa haitawezekana, jawabu halitakuwa kuendeleza utawala uliopo kwa kuongeza mihula ila kutafuta mtu aliye karibu zaidi na hulka hii, ikiwezekana ajifunze mengine akiwa madarakani au afanye mabadiliko kidogo. Hiyo pia haiwezi kuharibu chochote na katika msamiati wa kisiasa ni kama 'hewa mpya,' au ari mpya, kasi na nguvu mpya.

Mara nyingine utawala unapobadilika yanaweza kuwapo mageuzi ya kina yanayofanyika kwa dhamira njema na yanayofaa kufuatwa hata kama yanatuondoa katika yale tuliyozoea. Alisema Mwalimu Nyerere akiwa London mapema mwaka 1985 kuwa ni lazima aondoke madarakani aonyeshe utii kwa kiongozi mpya anayechukua nafasi yake, ili nchi ibaki katika umoja na mshikamano.

Kama alivyosema hayati Dk. Omar ni lazima kiongozi aondoke akiwa bado anapendwa, ili neno lake lisaidie kuweka mambo sawa pale ukinzani unapozuka katika utawala unaofuata. Akingoja kupigwa mawe hataweza kuwa na mamlaka ya uadilifu kuwaambia watu watulizane au waunge mkono kiongozi mpya anachofanya kwani itahatarisha amani.

# Kifo cha Seif kilivyozima ndoto za Lipumba

INATOKA UK. 11

vyama viliungana na kuanzisha UKAWA, bado vina nafasi ya kukutana na kujadili kwa kina jinsi ya kudai tume huru ya uchaguzi kwa pamoja badala CUF pekee kujitwisha mzigo huo," anasema Mrikaria.

Anahoji kuwa, vyama hivyo viliwezaje kuungana na kunzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi na sasa vinashindwaje? Anasema, ni muhimu kutafakari ni wapi vilikosea umoja huo ukasambaratika na kujipanga upya.

"Jambo la msingi ni viongozi kutanguliza maslahi ya taifa mbele badala ya vyama, ili hatimaye visiendelee kuwa vya kusindikiza katika uchaguzi mkuu kama ambavyo vimekuwa vikifanya," anasema.

Katibu huyo mstaafu anasema, mbinu zilizowezesha kuwanzishwa kwa UKAWA zitumike pia kushawishi vyama vya upinzani kuungana ili kuwa na nguvu za pamoja ambazo zitaviwezesha kudai tume huru.

"Lengo la chama cha siasa ni kushika dola kwa njia halali ya uchaguzi ili kujenga nchi, lakini hilo haliwezi kutumia iwapo vyama vitaendelea kutengana na kukumbatia migogoro," anasema.

Inamweleza Profesa Lipumba kuwa Maalim Seif alikuwa na uzito wake katika siasa za Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na kwamba amemaliza kazi yake kilichobaki ni wanasiasa kuiga mfano wake na kuonekana na umoja, nguvu na mshikamano zaidi kwenye kutetea maslahi ya taifa.

**AANGALIE WENGINE**

Mchambuzi wa siasa, Abdulkarim Atiki, anasema badala ya Prof. Lipumba kusubiri wanachama wa CUF waliohamia ACT-Wazalendo ili warudi wadai katiba mpya na tume huru kwa pamoja, apanue wigo ili kupata washirika wengine zaidi.

"Wakati CUF ikiwa imesusa kushiriki uchaguzi hadi iwepo tume huru ya uchaguzi na hata katiba mpya, ihamasishe wadau wengine wa siasa kufanikisha lengo hilo," anasema Atiki.



Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, akila kiapo cha kuanza majukumu mapya Ikulu jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Uteuzi Dk. Bashiru

## ■ Ashauriwa kuwalinda vyama vyote vya siasa

**Na Gaudensia Mngumi**

RAIS John Magufuli, amemteua Balozi Bashiru Ally, kuwa Katibu Mkuu Kiongozi kulisukuma taifa mbele kwenye zama ambazo kila kitu kinahusishwa na umahiri au 'smartness'. Duniani leo umahiri unatajwa kila mahali utasikia 'uongozi na uchumi mahiri bila kuzisahau simu ambazo ni 'smart phones', kutokana na umahiri ulio ndani ya vifaa hivyo.

Dk. Bashiru anasifiwa kuwa ni kiongozi mahiri ambaye kutokana na mahitaji ya wakati kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu Kiongozi kunaonyesha kuwa Rais amefanya chaguo linalokwenda na wakati.

"Amemchagua KMK ambaye anamudu mchakamchaka katika kufanyakazi zilizo mbele yake," ni kwa mujibu wa Abasi Mwalimu, mhadhiri na mchambuzi wa masuala ya kimataifa na kitaifa, anapozungumza na Nipashe mara baada ya uteuzi huo.

Dk. Bashiru aliyeteuliwa wiki iliyopita anachukua nafasi iliyoachwa na Balozi John Kijazi, aliyefariki wiki mbili zilizopita.

Mwalimu anamwona Dk. Bashiru kama kiongozi anayefaa kuwa mshauri mkuu wa Rais kutokana na uchapaji kazi wake unaoambatana na msimamo usioyumba, mtendaji kazi kwa weledi na mtetezi wa falsafa za siasa za ujamaa, uzalendo, haki, utu na ustawi wa watu na taifa.

Mchambuzi Mwalimu anasema KMK ni mchapakazi ambaye amekiongoza Chama Cha Mapinduzi (CCM) na sasa kimesimama na kinaheshimika.

Aidha, anaona kuwa kina maadili, upo uwajibikaji ndani ya chama, miradi na uwekezaji kwa tija pamoja na utendaji kazi unaojali wananchi ambayo ni mabadiliko yanayokifanya chama kiwe 'smart' zaidi jambo linalomwongezea sifa za utendaji Dk. Bashiru.

Katibu Mkuu Kiongozi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2002 kifungu cha 4 (1)-(4) ni mkuu wa utumishi wa umma, wakati katiba ya Tanzania ya 1977 ibara ya 60 inamtaja kuwa ndiye Katibu Mkuu wa Baraza la Mawaziri ambalo Rais ni Mwenyekiti.

Majukumu yake yanaonekana pia katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995 akitajwa kuwa ni msimamizi mkuu wa maadili ya viongozi wa umma.

Mwalimu anasema majukumu haya atayaweza kwa sababu ana msimamo usioyumba, ana maadili na kitakachomwongoza ni kutenda kazi kwa haki kwa kuzingatia utu, uzalendo na ustawi wa watu na taifa lao, lakini siyo kiongozi mwenye woga.

Anamtaja kuwa ana uwezo wa kumkemea na kumkosoa yeyote, iwe hadharani au kwa maandishi akikumbusha tukio la Katibu Mkuu Kiongozi wakati huo akiwa Katibu Mkuu wa CCM alipomwonya na kumwombea msamaha aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa kauli yake iliyokuwa inazungumzia masuala ya ukabila.

**MAHITAJI YA WAKATI**

Rais amemteua Dk. Bashiru katika kipindi ambacho watendaji wa aina yake ndiyo wanaohitajika, anasema Mwalimu.

"Ukiangalia zama hizi watendaji wakuu au makatibu wakuu wa aina yake ndiyo wanaochapakazi za kusimamia utendaji na uendeshaji wa shughuli zote za serikali kwenye wizara."

"Mathalani, kuna ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020, lakini pia ipo ya sasa ya 2020/25 zote zinatakiwa kufanyiwa kazi kwa vile kuna mambo mengi hayajatekelezwa. Ndiyo maana wanahitajika wachapakazi kama Dk. Bashiru wanaoweza kukimbia mchakamchaka muda wote. Kwani bila hivyo kazi zinaweza kukwama. Watendaji wa aina ya KMK ndiyo mahitaji ya wakati uliopo," anasema Mwalimu.

> Mambo kama hayo yawe ni darasa kwa CCM na kuhakikisha kero zote zinazowakabili Watanzania, zinapatiwa ufumbuzi, lakini viongozi wakibweteka na kuona ni jambo la kawaida, yaliyovikuta vyama vingine vikongwe yanaweza kutua katika chama hicho.

**UJASIRI**

KMK Bashiru ni jasiri asiyeogopa na amefanya mambo ambayo pengine wengine wangeyaogopa ikiwamo kazi ya kuongoza kamati iliyofuatilia mali za CCM, kuzihakiki na kuhakikisha kuwa zinarudishwa mikononi mwa chama.

"Hilo pekee limedhihirisha kuwa ni mtu jasiri, anayesimamia sheria, miongozo na taratibu mwenye sifa kubwa ya kufuatilia mwanzo hadi mwisho.

Akitoa maelekezo huwaachia wengine bado anakamilisha kazi. Ni lazima ajue hatima na iwapo lengo limetimia," anasema Naibu Katibu Mkuu wa CUF-Bara, Magdalena Sakaya.

Anasema Katibu Mkuu Kiongozi Bashiru ni mtu ambaye ana sifa zote za uongozi na anapotoa kauli zina mashiko. Tena zinazotingisha na zinazowafanya wengine kuwajibika au kuchukua hatua na hata kujisahihisha.

**WASIWASI WAKE**

"Ana sifa zote bora za uongozi na anastahili kuwa msaidizi wa Rais, lakini tunajiuliza atabadilika? Amekuwa na msimamo wa kichama muda wote, je, ataweza kuondoka kwenye uelekeo huo na kuanza kufanyakazi za kitaifa kwa ajili ya Watanzania wote?"

"Ninasema hivi kwa sababu jukumu alililo nalo Dk. Bashiru sasa ni la kitaifa ni mtendaji mkuu wa taifa siyo chama tena."

Naibu Katibu Mkuu wa CUF, anamshauri kubadilisha uelekeo na kukubali kuwa Tanzania ni taifa la vyama vingi na kuzikubali pamoja na kuzidumisha siasa za ushindani ili kuongeza ustawi wa demokrasia pamoja na kuwaletea wananchi maendeleo.

"Tunaomba akumbuke kuwa ni kiongozi wa taifa, wana CCM ni wake, wasio na vyama na wanachama wa vyama vya upinzani wote wanamtizama." Anasema Sakaya.

Sakaya ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Kaliua, anasema huo ndiyo wasiwasi wake wakati Dk. Bashiru anapoanza safari yake ya kuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Viongozi wengine waliowahi kushika wadhifa huo ni pamoja na Timothy Apiyo, wakati wa awamu ya kwanza, Marten Lumbanga, awamu ya tatu, Philemon Luhanjo na Balozi Ombeni Sefue wakati wa awamu ya nne na Balozi John Kijazi.

# NI OTHAM MASOUD

## •Amerejea kwa kasi, nguvu mpya

**Na Sabato Kasika**

MWANASHERIA mbobezi, Othman Masoud Othman, kutoka Chama cha ACT- Wazalendo, ameteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, kuziba nafasi iliyoachwa na Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia hivi karibuni.

Uteuzi huo ulifanywa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na tayari jana, kiongozi huyo ameshaapishwa kushika wadhifa huo.

Mwanasiasa huyo ambaye jina lake lilivuma wakati Bunge Maalum la Katiba lililokuwa linajadili rasimu ya katiba mpya mwaka 2014, uteuzi wake umefanyika baada ya kushauriana na chama chake.

Inaelezwa kuwa ametumikia serikali tangu kipindi cha kwanza chini ya mfumo wa vyama vingi akianzia na Dk. Salmin Amour Juma, kisha kwa Amani Abeid Karume mwaka 2000 hadi 2010 akiwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

Nafasi nyingine ambayo amewahi kushika ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kipindi cha Dk. Ali Mohammed Shein, lakini baadaye akaondolewa kwenye nafasi hiyo Oktoba mwaka 2014, baada ya kutofautiana na kupishana kauli.

Baadhi ya wachambuzi wa siasa, akiwamo Said Msonga, wamezungumzia uteuzi wa mwanasheria huyo huku akisema, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameteua mtu sahihi kwenye nafasi hiyo.

Msonga anasema, haijalishi amewahi kufukuzwa serikalini na kwamba jambo la msingi ni kuangalia anaweza kuwa na mchango kiasi gani kwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

"Nafasi hiyo imepata mtu sahihi, kwa kuwa si mgeni katika utendaji serikalini, amewahi kuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Sheria na Katiba na Utawala Bora Zanzibar, amekuwa DPP," anasema Msonga.

Anaongeza kuwa, amewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, na kwamba uzoefu mkubwa na sifa za kipekee, ambapo uzoefu wake katika utendaji serikalini unamfanya awe na sifa muhimu za kuwa mrithi wa Hamad.

"Huyo ni mwanasheria mbobezi ana msimamo kwenye maslahi ya Zanzibar, hivyo uteuzi huo utakuwa ni nafasi nzuri ya kumshauri rais katika mambo mbalimbali yakiwamo ya kisheria nayohusu maslahi ya Zanzibar," anasema.

Mwanasiasa Thomas Ngawaiya, aliyewahi kuwa Mbunge wa Moshi Vijijini (TLP) anasema, mteule huyo hajui ajenda ya Maalim Seif na kwamba ataungana na Dk. Mwinyi kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na kuijenga Zanzibar.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Othman Masoud Othman.

"Maalim Seif alikuwa na ajenda ya kuchimba mafuta yawe Wazanzibar tu, yaani kwa maana ya kuwekeza Zanzibar, na wafuasi wake walimwelewa, sina uhakika kama huyu mpya watamwelewa," anasema Ngawaiya.

Anafafanua kuwa, Maalim amewahi kuwa katika serikali kwa muda mrefu alikuwa akijua mambo mengi na kwamba alikuwa akichukua udhaifu wa serikali na kuchochea kwa wananchi na kupata umaarufu mkubwa.

"Kwanza kabisa nimpongeze Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini mtazamo wangu nilidhani nafasi hiyo ingechukuliwa na Juma Haji Duni," anasema Abdul Kambaya wa CUF.

Mjumbe huyo wa Baraza Kuu la Uongozi Taifa CUF, anafafanua kuwa kigezo alichokiona kwa Duni ni kwamba ni mwanasiasa pekee aliyepata misukosuko mingi tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa kuliko mwingine wote.

"Nilichobaini ni kwamba ACT-Wazalendo imetoa jina la Othman kutoka katika ngome yao kule Pemba, ingawa hajawahi kupata misukosuko mikubwa zaidi ya ule wa kufukuzwa uanasheria mkuu wa Zanzibar," anasema.

Hata hivyo, anasema, anatambua taaluma ya sheria ya Othman, kwamba ana uwezo mzuri wa kuuchambua Muungano, na kwamba uwepo wake katika SUK, utasaidia kuzipatia ufumbuzi zile kero za miaka mingi.

"Uzalendo wake kwa Zanzibar utamfanya awe maarufu katika siasa za visiwani na kushika nafasi kubwa ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuziba nafasi ya Maalim Seif," anasema.

### KWANINI ALIONDOLEWA?

Inaelezwa kuwa mwanasheria huyo, hakukubaliana na muundo wa serikali mbili hali iliyosababisha atofautiane na msimamo wa CCM katika baadhi ya vifungu vya rasimu ya katiba mpya.

Alisimamia muundo wa muungano wa serikali tatu, hali iliyomweka katika wakati mgumu bungeni na hatimaye kuenguliwa kwenye nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar.

Inaelezwa kuwa tangu alipofukuzwa katika nafasi hiyo ameandika makala nyingi katika tovuti na mitandao ya kijamii na kushiriki mijadala katika kumbi mbalimbali na mahojiano katika vyombo vya habari. Hatua hizo zinatajwa kuwa ni moja ya harakati za kutumia taaluma yake kutetea maslahi ya Zanzibar ndani ya Muungano, na kuendelea kujipatia umaarufu mkubwa kwenye siasa na hata katika jamii.

# Bil. 27.7/- kujenga zahanati 555

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 27.75 katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati mpya 555.

Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumzia jitihada za serikali katika kuboresha sekta ya afya ya msingi.

Alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya msingi katika mamlaka za serikali za mitaa.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Desemba, mwaka jana, serikali imetoa Sh. bilioni 386.8 kati ya hizo Sh. bilioni 312.3 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya.

"Pia Sh. bilioni 68.7 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na Sh. bilioni 5.8 kwa ajili ya uwekaji wa mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) na mafunzo kwa wataalamu wa kutoa dawa za usingizi na ganzi," alisema na kuongeza kuwa kwa kipindi hicho zahanati 1,198 zilijengwa.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha mwaka 2020/21, serikali imetenga Sh. bilioni 33.5 kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika hospitali mpya na Sh. bilioni 57, kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali hizo mpya na 71 zilijengwa awamu ya kwanza na 28 awamu ya pili.

"Hospitali za halmashauri zinazoendelea kujengwa mpaka sasa ni 102, ambapo hospitali tatu kati ya hizo zinajengwa kwa fedha za makusanyo ya ndani ya halmashauri," alisema.

Dk. Kapologwe alisema hospitali hizo tatu zinazojengwa kwa makusanyo ya ndani ni kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Jiji la Arusha, Mwanza na Manispaa ya Kinondoni (Mabwepande).

# Jafo awa mbogo miradi soko, kituo mabasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, ametoa siku 12 kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuhakikisha Soko la Ndugai na Kituo cha Mabasi yaendayo mikoani, vinafanya kazi kama ilivyokusudiwa kutokana na kutoridhishwa na utendaji kazi wake.

Agizo hilo alilitoa jana katika ziara yake ya kukagua utendaji kazi wa miradi hiyo ambayo ni ya kimkakati na kubaini baadhi ya maeneo bado hayana wafanyabiashara huku kukiwa na mwamko mdogo wa ufanyaji biashara kwenye eneo hilo.

Jago alisema serikali imejenga miundombinu hiyo ya mabilioni ya fedha kwa ajili ya wananchi, lakini ufanisi wake bado hauonekani na kutaka kukwa mbinu mbalimbali za kuongeza mwamko na mzunguko wa biashara kwenye miradi hiyo.

"Yaani kutoka hapa hadi mjini kati ni umbali wa kilomita nane, inashangaza kuona mradi huu ambao umekamilika kwa muda mrefu wa soko, lakini mwamko wa biashara hakuna na maeneo mengine bado hakuna wafanyabiashara, hii kwa kweli haijaniridhisha," alisema.

> **Kuna malalamiko kuhusu mageti na abiria kutembea umbali mrefu kutoka ndani hadi kwenye kituo cha daladala na mengine kidogo naagiza yashughulikiwe ili hawa wafanyabiashara wasipate kikwazo.**

Kutokana na hali hiyo, aliagiza Jiji hilo kuhakikisha malori yote ya mizigo ya masokoni kushusha kwenye soko hilo ili kuongeza mwamko wa biashara.

"Hili eneo la soko bado lipo wazi mmeshindwa nini siku zote kufanya? Nataka soko hili liwe 'busy', haiwezekani muwekewe miradi mikubwa ya gharama kubwa halafu haina watu, sijaridhishwa kabisa na hili soko hakuna kinachofanyika," alisema.

"Kodi zinazotozwa ziwe rafiki kwa wananchi maana hii miradi ni kwa ajili yao, soko hili limejengwa kwa fedha za serikali na si za mkopo hivyo msiwatoze fedha kubwa kama vile mnarejesha mkopo benki," aliongeza.

Akiwa katika kituo cha mabasi, Waziri Jafo aliitaka halmashauri hiyo kushughulikia kero zilizopo kwenye kituo hicho ili kifanye kazi kwa ufanisi.

"Kuna malalamiko kuhusu mageti na abiria kutembea umbali mrefu kutoka ndani hadi kwenye kituo cha daladala na mengine kidogo naagiza yashughulikiwe ili hawa wafanyabiashara wasipate kikwazo," alisema.

Pia aliagiza kuwekwe mashine za kukusanya mapato kwa kila geti ili kurahisisha utendaji kazi na ukusanyaji mapato kutokana na kwasasa watu wanaoingia kwenye kituo hicho kutumia geti moja na kuwa kikwazo kwao.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, aliahidi kushughulikia maelekezo ya Waziri huku akisema katika soko hilo ndani ya wiki mbili kunatarajia kuwekwa gulio na shughuli zingine za kiuchumi jambo ambalo litaongeza mzunguko wa biashara kwenye eneo hilo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema uongozi wa Mkoa utahakikisha shughuli za kibiashara kwenye maeneo hayo zinachangamka na hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kuleta ufanisi.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kushoto), akimsikiliza Mkuu wa Kituo cha Polisi Mpwapwa, mkoani Dodoma, David Kinyage, alipotembelea kukagua kituo hicho na kuzungumza na mahabusu jana. Katikati ni Kaimu Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mpwapwa, Maulid Manu. **PICHA: WMNN**

# Watakiwa kuchukua tahadhari magonjwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuchukua tahadhari na makundi ya waganga wa tiba asili na wapiga ramli wanaodai kutoa tiba ya ugonjwa wa corona.

Naibu Katibu Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Askofu Julias Bundala, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema ni vyema Watanzania wawe makini na watu hao wanaojitangaza kuwa na tiba hizo.

"Watanzania lazima tuwe makini hawa watu ambao wamekuwa na tabia ya kujitangaza kuwa wana dawa za tiba asili zinazoweza kuponya maambukizi ya virusi vya coroma kwani hali hii inaweza kuwapumbaza na kuacha kuchukua tahadhari za kulinda na homa hiyo ya mapafu," alisema.

Alisema kuwa kujitangaza kuwa wana uwezo wa kuponya maambukizi hayo watasababisha watu wengi kupoteza maisha yao.

Alibainisha kuwa ni muhimu sasa kwa Watanzania wakachukua tahadhari kwa kufuata maelekezo ambayo yanayotolewa na serikali.

Bundala alishauri viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu ili kusaidia serikali na waatalamu wa afya ambao wamekuwa wakitoa maelekezo jinsi ya kujilinda na tishio la ugonjwa huo.

Pia aliwataka Watanzania kuondokana na hofu kwa kuwa inaweza kuwasababishia kuibuka kwa magonjwa mengine.

Alisisitiza wananchi wanaofanya shughuli zao za kujiingizia kipato kwenye mikusanyiko wahakikishe wanajilinda kwa kufuata masharti ambayo wameelekezwa na wataalamu wa afya na viongozi wa serikali na wa dini.

"Kwenye maeneo yetu ya nyumba za ibada, majumbani mwetu sehemu zetu za kazi tuhakikishe tunajilinda kwa kuweka maji tiririka yenye sabuni, vitakasa mikono pamoja na kuvaa barakoa kwa ajili ya kujiwekea mazingira ya usafi," alisema.



HABARI MBEYA

# Bilioni 1.2/- kutumika mradi joto ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO) limeingia mkataba wa miezi mitatu na kampuni tanzu na Shirika la Umeme (TANESCO) ya uendeshaji wa joto ardhini (TGDC), kuchimba visima vitatu vifupi vya utafiti wa mradi wa joto ardhini.

Mradi huo utakaotekelezwa katika Kijiji cha Kyejo wilayani Rungwe mkoani Mbeya, una thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.2.

Mkataba huo ulitiwa saini juzi jijini Mbeya na unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi mitatu, ukitarajiwa kuwezesha kampuni ya TGDC kuanza kufanya utafiti wa joto ardhi na kuanza uzalishaji wa nishati ya umeme megawati 200 katika visima vitano vilivyochimba katika Wilaya ya Rungwe na Mkoa wa Songwe.

**Tayari walishafanya utafiti na kubaini kuna uzalishaji wa joto kwa asilimia 140 ambazo zitawezesha kuzalisha kiwango cha megawati 60 za nishati ya umeme.**

Meneja Mkuu wa TGDC, Kato Kabaka, alisema tayari walishafanya utafiti na kubaini kuna uzalishaji wa joto kwa asilimia 140 ambazo zitawezesha kuzalisha kiwango cha megawati 60 za nishati ya umeme.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Leonard Masanja, aliiagiza STAMICO kuharakisha kukamilisha mradi huo ili kuiwezesha jamii kunufaika na uzalishaji wa nishati ya umeme na kufikia malengo ya serikali ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

"Utendaji wa STAMICO ulisuasua kutokana na madeni ya zaidi ya Sh. bilioni moja na serikali imefanya jitihada za kuifufua ili fedha zitokanazo na miradi zitumike kwa ajili ya kusimamia kukamilisha miradi mingine na kutoa tenda za zabuni," alisema Masanja.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Venance Mwasse, alisema wanatarajia mradi huo kukamilika ndani ya siku 90 na kwamba watatumia vifaa vya kisasa kuchoronga visima hivyo ili TANESCO ianze utekelezaji wa uzalishaji wa nishati ya umeme.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Meja Jenerali mstaafu, Hamis Semfuko, akizungumza na watumishi wa Pori la Akiba la Mpanga/Kipengere, wilayani Makete, mkoani Njombe juzi, kwa lengo la kukuza na kutunza uhifadhi wa wanyama. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'TAWA ihakikishe mapori yanainua uchumi'

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), Meja Jenerali Hamis Semfuko, amewaagiza watumishi wa mamlaka hiyo kusimamia na kulinda mapori yote ya akiba, ili kuchochea uchumi na kukuza utalii kupitia sekta hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na watumishi wa mamlaka hiyo alipotembelea Pori la Akiba Mpanga/Kipengere lililoko kwenye mikoa ya Mbeya na Njombe.

Meja Jenerali Semfuko alisema moja ya mikakati ya TAWA ni kusimamia na kuboresha maeneo yote ya mapori yote ya akiba, ili kuvutia watalii kutoka ndani na nje ya nchi.

"Tutahakikisha TAWA imeweka mazingira rafiki ya kuvutia watalii ili kuongeza pato la taifa kupitia uhifadhi na katika kufanikisha hilo, watumishi wote wameongeza usimamizi na udhibiti hususani wavamizi wa mapori pamoja na majangili," alisema.

Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alisema wanafanya ukaguzi katika uendelezaji wa miradi ya maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya utalii na ufuatiliaji kupitia mapori ya akiba na vivutio vingine vya utalii vinavyomilikiwa na mamlaka hiyo.

Kamishna Nyanda alisema watahakikisha wanaimarisha uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na kuongeza watalii, ukusanyaji wa mapato na kuboresha utendaji wao.

Meneja wa Pori la Akiba Mpanga/Kipengere, Joas Makwati, alisema eneo hilo ni miongoni mwa maeneo yenye vivutio vya utalii kutokana na kuwapo kwa aina mbalimbali za wanyamapori na maporomoko saba ya maji yakiwamo ya Kimani ambayo yana upekee katika ukanda wa kusini mwa Tanzania.

Alisema miongoni mwa vikwazo katika uhifadhi wa maeneo hayo, ni uhaba wa watumishi, ukosefu wa kambi za kitalii na barabara za kuvifikia vivutio.

# Maji yasababisha wanawake kupigwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wanawake katika Kijiji cha Swaya wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wamedai ukosefu wa maji katika kijiji hicho umekuwa ukisababisha vipigo kutoka kwa waume zao wanapochelewa kutoka kutafuta huduma hiyo.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo jana, wanawake hao walidai kata nzima ya Swaya haina hata kijiji kimoja chenye maji ya bomba na hivyo wanategemea maji ya chemchemi.

Mmoja wa wanawake hao, Sabina Mwalosi, alisema kutokana na tatizo hilo, wanalazimika kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo na wamekuwa wakihisiwa na waume zao kuwa badala ya kuchota maji, wanatumia muda huo kufanya starehe na wanaume wengine.

"Wakati mwingine huwa tunarudi saa nne au saa tano usiku kutoka kwenye maji, lakini wanaume huwa hawaamini kuwa tulikuwa kwenye maji na badala yake huwa wanadhani tulikuwa kwenye michepuko, kwa hiyo wanatupiga," alisema Sabina.

Alisema wanakijiji walikubaliana kuchangishana fedha kwa ajili ya kujenga mradi wa maji, lakini kutokana na tatizo la kiuchumi, wameshindwa kuukamilisha.

Sabina aliiomba serikali kuwasaidia kukamilisha mradi huo, ili waondokane na tatizo hilo ambalo linasababisha migogoro ya kifamilia na hata kuvunjika kwa ndoa.

Tumpe George, mwanakijiji mwingine, alisema uhaba wa maji kwenye eneo hilo unasababisha uhasama hata baina ya wanawake wenyewe kwa kuwa huwa wanagombana wanapochota maji hayo kwa kila mmoja kutaka atangulie kuchota.

Alisema mradi wa kijiji ukikamilika, watakuwa wamekombolewa na watautumia muda wao mwingi kwenye shughuli za uzalishaji badala ya kutafuta huduma hiyo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Swaya, Fred Sashe, alikiri kuwapo kwa tatizo la maji na migogoro ya ndoa ambayo inasababishwa na tatizo hilo.

Alisema wanafanya kila jitihada kuhakikisha huduma ya maji ya uhakika inakuwapo kijijini huko.



## Waumini wa dini zote watakiwa kuimarisha ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi B Unguja, Hamida Mussa Khamis, amewataka waumini wa dini ya Kikristo wa Kanisa la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mwanakwerekwe, kuimarisha ushirikiano na uhusiano mzuri baina yao na waumini wa dini nyingine.

Alisema uhusiano baina ya wananchi wanaoishi katika maeneo jirani ya kanisa hilo utasaidia kila mmoja kutekeleza haki ya msingi ya kuabudu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa kanisa hilo pamoja na wananchi wanaoishi jirani na eneo la kanisa hilo kufuatia kuwapo kwa malalamiko ya uwekwaji wa sauti ya juu kwa vipaza sauti katika siku ambazo sio za ibada.

Alisema waumini wote wanapaswa kuwa na ushirikiano na uvumilivu wa kidini na kila mmoja anapaswa kujali na kuheshimu dini ya mwingine.

Aliwataka kufuata miongozo yote iliyotolewa na serikali wakati wa ibada ili kutowabugudhi watu wengine.

Naye Mchungaji wa Kanisa hilo la KKKT Mwanakwerekwe, Shukuru Maroda, alisema anaushukuru uongozi wa wilaya kwa kuwakutanisha pamoja na wakazi jirani wa eneo hilo na kufikia muwafaka katika mazungumzo hayo.

Alihakikisha kufuata miongozo ya kufanya ibada bila kuleta usumbufu kwa watu wengine na kuimarisha uhusiano kati yao na wananchi wanaoishi maeneo jirani ya kanisa hilo bila kuathiri imani zao za kidini.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi wanaoishi jirani na kanisa hilo walisema wanathamini kuwapo kwa kanisa hilo katika maeneo hayo bali waumini hao wanapaswa kufuata taratibu za kisheria za ufungaji wa vyombo vya muziki na vipazo sauti vinavyotumika wakati wa ibada.

# Ampongeza Masoud kumrithi Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Jimbo la Gando Pemba, Salim Mussa Omar, amepongeza uteuzi wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar wa Othman Masoud kwa kuwa ni mtu mkarimu na asiyependa makuu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufariki kwa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad.

Aliwataka wananchi kuvumiliana na kuweka pembeni mihemko ya kisiasa ili kujenga nchi na kuendeleza maridhiano na kusonga mbele kimaendeleo.

**Rushwa sio jambo la kuondoka kwa ghafla hata nchi zinazoendelea rushwa ipo hivyo ni vyema elimu ya rushwa kuanza kutolewa shuleni.**

Akizungumzia kuhusu rushwa ambayo Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi anapambana nayo, alisema ili kutokomeza rushwa ni lazima kuwatengeneza watoto kuanzia shuleni na wanapokuwa watumishi wasijihusisha na vitendo hivyo.

"Rushwa sio jambo la kuondoka kwa ghafla hata nchi zinazoendelea rushwa ipo hivyo ni vyema elimu ya rushwa kuanza kutolewa shuleni," alisema.

Alisema kuwa rushwa ni adui wa haki na itarejesha nchi nyuma kimaendeleo na kusababisha mtu ambaye anastahiki kupata alama ya kwanza akapata ya mwisho na wa kupata alama ya mwisho akapata ya kwanza.

Alisema ni vyema kumuunga mkono Rais wa Zanzibar Dk. Mwinyi na kumwonea huruma kuwa anapambana na jambo zito la rushwa.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuwa wastahamilivu pale mmoja wao anapokamatwa na rushwa na kuchukuliwa hatua stahiki na kuacha kuoneshana vidole.

"Tuvumiliane tunajua kuwa Wazanzibari sote ni ndugu na hili ni jambo zito linalomkumba Rais...kila mmoja atakula alichokipanda," alisema.



Wataalamu wa kilimo wa kisiwa cha Pemba, wakiwa katika mafunzo ya mbinu bora za kuwafundishia wakulima wa kilimo cha viungo, yaliyofanyika kisiwani humo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yatoa mkono wa pole kwa ACT -Wazalendo

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Saadalla (Mabodi), amewataka viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki cha kufiwa na Mwenyekiti wao, Maalim Seif Sharif Hamadi.

Aliyasema hayo, alipofika na ujumbe wa Sekretarieti ya chama hicho kwa upande wa Zanzibar, kutoa mkono wa pole kwa uongozi wa chama hicho katika ofisi kuu, Vuga Wilaya ya Mjini, Unguja.

Alisema msiba wa Maalim Seif ni wa taifa zima na sio chama pekee na kwamba kiongozi huyo alikuwa ni msingi wa maendeleo yaliyofikiwa sasa, na kushauri kuendelea kuyatunza maridhiano yaliyofikiwa na viongozi hao.

"Maalim Seif ni miongoni mwa viongozi na mwanasiasa mkongwe ambaye enzi za uhai wake alikuwa ni mpenda maendeleo na aliyependa uwajibikaji katika maeneo ya kazi," alisema.

Alisema CCM itaendelea kukumbuka mchango alioutoa makamu huyo katika serikali kwa kuwa alikuwa akishirikiana na viongozi waliokuwapo maradakani kutoka kwenye chama hicho.

Alisema katika uongozi wake Maalim Seif alitafuta miafaka ya kisiasa kwa lengo la kuwaunganisha wananchi ili nchi isiingie katika machafuko.

Alihakikisha kuwa CCM ipo tayari kukaa meza moja na ACT-Wazalendo kujadili masuala ya kisiasa hasa maendeleo ya nchi na kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watayatekeleza na kuyasimamia.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa ACT -Wazalendo Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, kwa niaba ya chama chake, alisema wamepokea mkono wa pole na wamefarijika kuona mchango mkubwa wa maridhiano ulioachwa na marehemu Maalim Seif umeanza kuzaa matunda.

Aliahidi kuendelea kudumisha maridhiano yaliyofikiwa na kiongozi wake na kuahidi kutoa mchango kadri utakavyowezekana katika kuleta maendeleo ya wananchi.

"Siku zote Mwenyekiti alikuwa akituhimiza umoja tuliokuwa nao tuendelee nao na maridhiano haya tuyadumishe, hivyo tunaahidi kufuata fikra zake ili maendeleo yafikiwe kwa pamoja," alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Zanzibar, Juma Duni Haji, alisema, kifo cha Maalim Seif kimewagusa wengi, lakini umoja na mshikamano aliouanzisha kiongozi huyo utaenziwa daima.

Wakati huo huo, uongozi ulifika kwa Mjane wa Maalim Seif, Sharif Mama Awena huko Mbweni nje kidogo na mji wa Zanzibar na kumuahidi kudumisha mambo mema yaliyoasisiwa na kiongozi huyo enzi za uhai wake, kuwaomba wanafamilia kuendelea kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu cha kuondokewa na mpendwa wao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAJI KHAMIS IDI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 419 ACG** SUZUKI ESCUDO. Chassis namba **TD01W130805.** Engine namba **G16A-302583.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/OST/RB/3884/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SEBASTIAN JOHN LUENA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **BMW** yenye namba za usajili **T450 DTS** chasis namba **WBAUF520X0PM72320** engine namba **N46B20BAO90H233,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/119887/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NO. 206/2019**
**MDAI SAMWEL KIARIRO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA MUSSA DAUDI MWAWOYA**
**Ombi la Mdai SAMWEL KIARIRO**
**Madai ya PIKIPIKI**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 17 mwezi 03 mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi.

**Angalia** kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Màhakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 23 mwezi 2 mwaka 2021

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**

**EXECUTION NO 80 OF 2016**
**Originating from taxation cause 80/2016**

**CHARLES NAIBALA………………..APPLICANT**
**VERSUS**
**THOMAS MARKO NAIBALA……...RESPONDENT**

**NOTICE TO MENTION**

**TO. THOMAS MARKO NAIBALA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court at Arusha on 6th day of APRIL, 2021 AT 09:00am in the forenoon.

YOU may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention,the court may proceed in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 02nd day of MARCH,2021

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Saudia yataka watakaohiji kupewa chanjo ya corona

**Riyadh,** SAUDI ARABIA

SAUDI Arabia imetangaza kuwa ni sharti la msingi kupigwa chanjo dhidi ya corona kwa ajili ya kufanya hija, mwaka huu.

Kulingana na gazeti la Ukaz, Waziri wa Afya, Tawfig Al-Rabiah, alisema kwamba ni lazima kuwa umepigwa chanjo ya Covid-19 kwa wale ambao wanataka kushiriki katika hija.

Waziri huyo alisema kwamba agizo hilo ni moja ya masharti ya kushiriki hija mwaka huu, Saudi Arabia.

Waziri Rabiah aliomba maandalizi ya mapema yafanyike kwa kuajiri wataalamu wa huduma ya afya kufanya kazi katika vituo vya afya, Mecca, Medina na maeneo matakatifu.

**Tumelisikia agizo hilo, lakini kwa sasa hatuwezi kusema chochote ni watu maalum ambao huandaa safari hizo.**

Iliarifiwa pia katika habari kwamba waziri aliamuru kuundwa kwa tume ya Covid-19 kwa mahujaji.

Nipashe jana, ilimtafuta Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi kuhusu suala hilo, alisema kwa upande kuna kamati ambayo hushughulikia suala la hija na hivyo kwa hivi sasa hakuna tamko.

"Tangu tulipoipata taarifa tulianza kufuatilia. Tumelisikia agizo hilo, lakini kwa sasa hatuwezi kusema chochote ni watu maalum ambao huandaa safari hizo.

Huwa kuna mawasiliano kati ya nchi mbili, Saudia Arabia na sisi kabla ya kwenda kuhiji. Kwa hiyo kwa sasa tusubiri."

Juni mwaka jana, Shirika la Utangazaji Uingereza (BBC), lilisema Saudi Arabia iliweka maarufuku raia kutoka mataifa mengine kufanya ibada ya Hija nchini humo ili kudhibiti virusi vya corona.

Idadi ndogo ya watu wanaoishi katika ufalme huo walishiriki Hija, kulingana na tangazo lililotolewa kwenye vyombo vya habari vya taifa hilo.

Mwaka jana ilikadiriwa watu takriban milioni mbili wangetembelea Mecca na Medina, msimu wa kiangazi kwa ajili ya Hija. **TRT/ NIPASHE**

## Okonjo-Iweala aahidi mabadiliko WTO

**Geneva,** USWISI

MKURUGENZI Mkuu Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala ameahidi kufanya kila awezalo kuleta mabadiliko.

Okonjo-Iweala ambaye anakuwa mkurugenzi wa saba kushika nafasi hiyo, na mwanamke Mwafrika wa kwanza kushika wadhifa huo, alianza kazi WTO juzi.

Alisema kuwa ana kibarua kikubwa cha kufanya na anahisi yuko tayari. Siku ya kwanza ofisini alikutana na wakurugenzi mbalimbali na wafanyakazi wengine wa shirika hilo, kula kiapo na kutia saini ya kuahidi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Alilishukuru baraza kwa kumwamini na kumuweka mamlakani, na kwamba atatumia uwezo wake wote, ikiwamo ujuzi, elimu na uzoefu kuleta mabadiliko.

"Tunapaswa kuwajibika zaidi kwa watu tunaowahudumia. Tumekuja hapa kuhudumia, watu wa kawaida wanawake na wanaume na watoto wetu ambao wanatumai kazi yetu.

Kusaidia mfumo wa kimataifa wa biashara italeta mabadiliko ya kweli katika maisha yao, itaboresha hali ya maisha na kuunda ajira kwa wanaotafuta kufanya kazi." **UN**

## WHO: Hatujui lini corona itakwisha

**Geneva,** USWISI

MKURUGENZI wa Programu ya Hali ya Dharura ya Shirika la Afya Duniani, Mike Ryan alisema kuwa si kweli kwamba, kuna matarajio ya kumalizika kwa virusi vya corona mwisho wa mwaka.

Mkurugenzi Mkuu wa (WHO), Tedros Ghebreyesus alifanya mkutano wa video kwenye makao makuu ya shirika huko Geneva, Uswizi.

Ghebreyesus alisema kuwa kesi za maambukizi zimeongezeka kwa mara ya kwanza wiki iliyopita, baada ya kupungua kwa wiki saba.

Mike Ryan: Ni mapema mno kuongelea kumalizika kwa janga mwishoni mwa mwaka 2021. Sio kweli. Alisisitiza kuwa WHO inazingatia kuzuia kuenea kwa virusi, Ryan alisema,

"Suala ni kwamba tunaweza kudhibiti virusi lakini kwa sasa vimezidi."

Mkurugenzi Mkuu wa (WHO) Tedros Ghebreyesus alifanya mkutano wa video kwenye makao makuu ya shirika huko Geneva, Uswizi. Ghebreyesus alisema kuwa kesi za maambukizi zimeongezeka kwa mara ya kwanza wiki iliyopita baada ya kupungua kwa wiki saba. **TRT**



Wasichana 279 waliotekwa nyara na watu wenye silaha kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Serikali, huko Jangebe, wiki iliyopita, wakiwa kwenye mkutano na Gavana wa Jimbo la Zamfara, Bello Matawalle, Gusau, Kaskazini mwa Nigeria, jana. **PICHA: AP**

## Sarkozy ahukumiwa kifungo miaka 3

**Paris,** UFARANSA

RAIS wa zamani wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy amehukumiwa kifungo cha miaka mitatu, baada ya kukutwa na hatia ya ufisadi na kueneza ushawishi.

Hukumu hiyo iliyotolewa jana na mahakama mjini Paris inajumuisha, mwaka mmoja gerezani na miaka miwili ya kifungo cha nje.

Sakorzy alikuwa anashtakiwa kwa kujaribu kupata taarifa za ndani kinyume cha sheria kuhusu uchunguzi juu ya ufadhili wa kampeni zake kutoka kwa jaji mwaka 2014.

Mahakama hiyo ilisema Sarkozy atakuwa na haki ya kuomba kuzuiliwa nyumbani kwa kutumia bangili ya umeme.

Washtakiwa wenzake wawili ambao ni wakili Thiery Herzog na Jaji Gilbert Azibert, pia walikutwa na hatia na wamehukumiwa kifungo sawa na chake.

Baadaye mwezi huu, Sarkozy atakabiliwa na kesi nyingine pamoja na watu wengine 13 kwa mashtaka ya kufadhili kinyume cha sheria kampeni yake ya urais mwaka 2012. **DW**

## Wasichana waliotekwa wakutana na Gavana

**GUSAU,** Nigeria

WASICHANA wa shule waliotekwa Nigeria na kuachiliwa na watekaji nyara wamekutana na gavana.

Gavana wa Jimbo la Zamfara, Bello Matawalle, alikutana na kikundi cha wanafunzi hao waliokuwa wametekwa nyara Ijumaa, katika shule ya bweni.

Wasichana 279 walipelekwa katika ofisi ya gavana katika mji mkuu wa jimbo Gusau kwa ajili ya kupatiwa maelezo.

Gavana Matawalle aliiambia BBC kuwa wasichana hao waliachiliwa baada ya kufanya mazungumzo na wanamgambo wenye silaha. **BBC**

# GUNDOGAN NUSURU ATUE MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

ILKAY Gundogan amefichua kwamba, Manchester United ilikuwa timu ya kwanza kutaka kumleta kwenye Ligi Kuu England, mara kadhaa kabla ya kusaini dili la kuwachezea wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City.

Kiungo huyo raia wa Ujerumani, Gundogan yupo kwenye kiwango bora kabisa kwa soka lake kwa sasa, akifunga mabao 11 katika mechi 19 za ligi.

Ubora wake ndani ya uwanja, unamfanya Gundogan kuwa mmoja wa wachezaji wanaopewa nafasi kubwa ya kushinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu, huku Man City ikionekana kuwa na nafasi kubwa ya kutwaa taji la ligi mara ya tatu katika kipindi cha misimu minne.

Huu ni msimu wa tano kwa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30 tangu alipotua England, akikipiga huko Etihad alikonaswa akitokea Borussia Dortmund mwaka 2016.

"Kabla ya kutua Manchester City, nilikuwa na nafasi ya kujiunga na Manchester United, lakini mpango huo haukukamilika," amesema akinukuliwa na Bild.

"Lakini tangu nimetua hapa, nafurahia maisha ya kila kitu kilichopo. Lakini naamini mambo yangekuwa tofauti kama ningekuwa kikosi cha Man United."




# *Pirlo: Hakuna kukata tamaa ubingwa Juve*

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo amesema kwamba, wachezaji wa Juventus bado wanaamini kuwa wanaweza kutwaa taji la 10 mfululizo la Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu.

'Bianconeri' hao wako nyuma kwa vinara Inter Milan kwa tofauti ya pointi 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa nafasi ya tatu.

Lakini Pirlo kabla ya mchezo wake wa jana, Jumanne dhidi ya Spezia alisema ana uhakika wachezaji wake watapambana kwenye mbio za ubingwa huo.

Juve hawajashinda katika michezo yao mitano iliyopita kwenye mashindano yote.

Licha ya pengo la Inter, Pirlo amesisitza kuwa kikosi chake hakijakata tamaa ya kunyakua Scudetto kwa mara nyingine.

"Bado tuna nafasi kwenye mbio za ubingwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Najua vijana hawa wanaamini, wanafanya mazoezi vizuri na wanataka kurudi kushinda taji na hii inanifanya nijisikie raha.

"Hatuangalii ni nani aliye juu yetu au nyuma yetu, tunakaza sisi wenyewe. Lengo lazima libaki vile vile. Kuna michezo mingi bado, tutakuwapo. "Lengo la awali lilikuwa kuwashinda wote, tunajua tulipoteza alama chache, lakini hiyo ni ya zamani. Lazima tuangalie mchezo ujao ni Spezia."

Juve imeshinda mara 21 kati ya mechi 23 za nyumbani za Serie A dhidi ya timu zilizopanda daraja.

# Moses amtaja Conte kocha bora kwake

**MOSCOW,** Urusi

VICTOR Moses amesema Antonio Conte ndiye kocha bora aliyewahi kufundishwa naye huku akibainisha kuwa angeweza kurejea Inter Milan.

Conte alimfundisha Moses wakati wa miaka yake pale Chelsea na sasa nyota huyo wa kimataifa wa Nigeria, anacheza kwa mkopo kule Spartak Moscow akitokea Chelsea, na alitumia miezi sita kucheza kwa mkopo Inter msimu uliopita.

"Conte ndiye kocha bora zaidi ambaye nimekuwa naye," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, akinukuliwa na Spartak.com.

"Alinisaidia kujiamini. Na ukweli ni katika kubadili mtazamo, si kwa sababu nilipata nafasi mpya upande wa kulia."

"Nilikuwa tayari kurudi (Inter) kabla ya kujiunga na Spartak. Nilikuwa tayari nimejadili kila kitu na Conte. Lakini mambo yakabadilika. Labda hali ya kifedha, lakini sijui.

"Wakati fulani, wakurugenzi wa Spartak wamewasiliana na mawakala wangu. "Marina Granovskaya alizungumza na wakala wangu na kuelezea ni kwa nini Spartak ilikuwa chaguo bora."



HABARI MICHEZO

# Lukaku apotezea mbio Kiatu na Ronaldo Serie A

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amesema kuwa hafikirii katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu na Christiano Ronaldo, licha ya kufikisha mabao 18 katika Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu nyuma ya Ronaldo mwenye mabao 19.

Mchezaji huyo raia wa Ubeligiji kwa mara nyingine alihusika kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Genoa na sasa amefunga katika michezo mitatu mfululizo ya 'Nerazzurri' hao.

Hajaenda bila kufunga kwenye michezo zaidi ya miwili kwa msimu huu katika kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte ambacho kina matumaini ya kushinda taji la Serie A, wakati huu kikiongoza msimamo wa ligi hiyo.

"Tumeimarika sasa, tupo juu kwenye msimamo wa ligi ni hisia nzuri, lakini lazima tuendelee kucheza kwa bidii," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Tulikabiliana na vipigo katika michezo kama hii msimu uliopita, kiukweli nina furaha sana kwa ushindi, sasa tunafikiria kwa mchezo ujao dhidi ya Parma hautakuwa rahisi.

"Tunataka kuwaonyesha wapinzani kwamba tupo hapa, tunawaza michezo inayokuja, ilikuwa ni mechi muhimu baada ya kushinda michezo miwili mfululizo.





# KEANE AKERWA NA KIWANGO MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

ROY Keane ameelezea kusikitishwa kwake na ukosefu wa ubora unaoonekana katika kikosi cha Manchester United baada ya sare ya bila kufunga na Chelsea, Jumapili.

Chelsea walionekana kuwa bora siku hiyo, na ingawa timu ya Ole Gunnar Solskjaer ilikuwa na wakati wake pia, hakuna ulinzi uliovunjwa pale Stamford Bridge.

Seti zote mbili za washambuliaji hazikufurahia kile walichokifanya, na gwiji huyo wa Man United, Keane alizungumzia mechi hiyo kama "yenye kuchosha" baada ya filimbi ya mwisho.

Akizungumza na Sky Sports, Keane alisema: "Ulikuwa mchezo mbaya, nilikuwa nikikasirika zaidi kadri mchezo unavyoendelea.

"Hakuna kujituma kuingia kwenye boksi. Ukosefu halisi wa ubora kwa United. Michezo mikubwa ambayo haizalishi mabao, hiyo lazima ilete wasiwasi.

"Wanajaribu kushinda, lakini michezo hii nadhani mawazo yao ni kwamba tusifungwe. Nadhani United wanaangalia timu zilizo nyuma yao kuliko kujaribu kushinda mechi na kuifukuzia Manchester City."

Kwa mujibu wa Keane, unapokuwa kwenye moja ya timu kubwa jukumu la kushinda mechi ni jambo muhimu zaidi.

# Liverpool yaifungia kazi saini ya De Paul

**LIVERPOOL,** England

IMERIPOTIWA kwamba, Klabu ya Liverpool inawania saini ya kiungo wa Klabu ya Udinesse ya nchini Italia, Rodrigo De Paul, ili ajiunge ndani ya kikosi hicho cha Ligi Kuu England.

Mbali na Liverpool kuwania saini ya nyota huyo raia wa Argentina ambaye anacheza ndani ya Serie A, pia Klabu ya Inter Milan nayo inatajwa kuwania saini yake.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, anaonekana kuwa bora ndani ya uwanja jambo ambalo limewafanya Liverpool wavutiwe naye na wapo tayari kuweka mkwanja mezani ili kupata saini yake.

Dau ambalo Liverpool inatajwa wameweka mezani ni euro milioni 30 kupata saini ya nyota huyo ambaye kwa msimu huu wa 2020/21 amecheza jumla ya mechi 23 na amefunga mabao matano na pasi tatu za mabao.

Kwa mujibu wa ripoti, Liverpool wapo tayari kutoa kiasi hicho, ili kuhakikisha nyota huyo anatua pale kwenye viunga vya dimba la Anfield.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HUGHES AIPELEKA UTD KWA KANE, HAALAND

**Watatakiwa kuingia sokoni, kutafuta wachezaji kama hao, na naamini wanaweza...**

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inatakiwa kumsajili Harry Kane au Erling Haaland ili kumaliza tatizo la nafasi ya ushambuliaji wa kati, kwa mujibu wa gwiji wa klabu hiyo Mark Hughes.

**United ndio timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu England msimu huu ikiwa na mabao 53, lakini wamekuwa na tatizo kwenye safu yao ya ulinzi kwa baadhi ya mechi.**

'Mashetani Wekundu' hao walitoka sare ya bila kufungana na Chelsea pale katika dimba la Stamford Bridge Jumapili na ilikuwa sare yao ya nne ya bila mabao wakicheza ugenini dhidi ya timu sita za juu.

Edinson Cavani alisajiliwa kwa uhamisho huru mapema msimu huu na amekuwa na kiwango cha kuvuti katika safu ya straika wa kati, lakini mchezaji huyo raia wa Uruguay umri unamtupa mkono, kwani sasa ana miaka 34.

Marcus Rashford, Anthony Martial na Mason Greenwood wote wamejaribu kuchezeshwa mbele katikati, lakini Hughes - ambaye alifurahia mafanikio hapo Old Trafford kati ya mwaka 1980-1986 na 1988-1995 - anaona timu hiyo bado haina straika wa kati.

Na anafikiri kwamba, nyota wa Tottenham, Kane na mkali wa Borussia Dortmund, Haaland ndio wachezaji wanaotakiwa kwenye kikosi cha Ole Gunnar Solskjaer.

"Nimeiona United mara nyingi na wana wachezaji wenye ubora. Rashford na Greenwood wapo vizuri," alisema akiiambia Sky Sports.

"Kwa upande wangu, wanamhitaji Cavani wa miaka mitano iliyopita wakati akiwa kwenye ubora wake; pengine walimsajili wakati ambao si sahihi kwao.

"Bado ni mshambuliaji mzuri wa kati. Wakati ukimwona yeye kwenye timu, nafikiri anaifanya timu pinzani kuwa na woga kidogo. Anaifanya timu ijiamini kucheza."

Alipoulizwa kama Kane au Haaland ndio jibu la matatizo ya United katika nafasi ya straika wa kati, Hughes alijibu: "Wao ni aina ya wachezaji wanaowahitaji kwa sasa.

"Watatakiwa kuingia sokoni, kutafuta wachezaji kama wale, na naamini wanaweza kufanya hivyo."

## ZISIKUPITE

### LACAZETTE KUONDOKA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kuondoka Arsenal mwishoni mwa msimu huu. ***(Football London)***

### 'UNITED HAIVUTII WACHEZAJI'

KLABU ya Manchester United haivutii tena wachezaji nyota duniani, kwa mujibu wa mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo, Andy Cole. Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 49, ameongeza kuwa Man United huenda ikamkosa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

### RICHARDS HUYOOO BAYERN

MLINZI wa kushoto wa klabu ya Reading, Omar Richards mwenye umri wa miaka 23, atajiunga na Bayern Munich kwa mkataba wa miaka minne mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### ABRAHAM ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham wana matumaini ya kumsajili mshambuliaji, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, kutoka Chelsea mwishoni mwa msimu huu. ***(Star)***

### CAHILL HANA WASIWASI

GARI Cahill mwenye umri wa miaka 35, amesema hana wasiwasi kuhusu hatima yake ya baadaye katika klabu ya Crystal Palace, licha ya kwamba mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Evening Standard)***

### HATIMA YA KANE KUJULIKANA

"MBIVU au mbichi" itajulikana kipindi cha majira ya joto, kama mshambuliaji, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, ataondoka Tottenham, amesema kiungo wa kati wa zamani wa Spurs, Danny Murphy. ***(Talksport)***

### MESLIER KUONDOKA LEEDS

GOLIKIPA Illan Meslier mwenye umri wa miaka 20, huenda akaondoka Leeds kama timu hiyo haitakuwa kwenye kiwango bora, amesema kiungo wa kati wa zamani, Danny Mills. ***(Football Insider)***

### CARLO HAKUMTAKA DOUCOURE

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, amesema kiungo wake wa kati, Abdoulaye Doucoure mwenye umri wa miaka 28, hakuwa katika orodha ya wachezaji aliotaka kuwasajili. ***(Goal)***

### EDOUARD AGOMBEWA EPL

KLABU ya Leicester City huenda ikakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal na Aston Villa katika mbio za kumsaka mshambuliaji wa zamani wa Celtic na Ufaransa, Odsonne Edouard, 23. ***(Leicester Mercury)***

### GARCIA KUTUA BARCELONA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema mlinzi wake, Eric Garcia, 20, atajiunga na Barcelona kipindi cha majira ya joto. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

## Kagera Sugar, Azam ni vita leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Azam FC, kipo tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu dhidi ya Kagera Sugar leo ili kuendelea kujiweka katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara, kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema wameenda kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo ili kujiweka katika nafasi nzuri kufikia malengo yao.

Alisema kikosi chao kipo vizuri na wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata matokeo, licha ya kwamba wanawaheshimu wapinzani wao.

"Tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo chanya, utakuwa mchezo wa ushindani kwa upande wetu tunatafuta pointi tatu, ligi imekuwa na ushindani mkubwa," alisema Vivier ambaye leo watakuwa na kazi ngumu katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

## Ihefu FC itabaki Ligi Kuu Bara - Katwila

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU kikosi chake kikishika nafasi ya tatu kutoka mkiani mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara inayoshirikisha timu 18, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema licha ya ushindani kuwa mkubwa ndani ya uwanja, watapambana kufanya vizuri ili kusalia katika ligi hiyo msimu ujao.

Ikiwa katika nafasi ya 16, baada ya kucheza mechi 21, Ihefu FC imejikusanyia alama 20 tu na leo itakuwa nyumbani jijini Mbeya kuikaribisha Gwambia FC ya Misungwi, Mwanza.

Timu nne msimu huu zitashuka daraja kwa zile ambazo zitashika nafasi ya 15 mpaka ya 18 huku zile za nafasi ya 16 na 17 zikicheza mechi za mchujo (play off) na timu mbili zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza.

Akizungumza na mwandishi wetu, Katwila alisema tayari wachezaji wameanza kuelewa kile ambacho wanafundishwa jambo linalowapa imani ya kubaki ndani ya ligi hiyo.

"Ukweli ushindani umekuwa mkubwa sana na kila timu inahitaji kufanya vizuri, hilo lipo wazi hata sisi pia tunapambana kupata matokeo chanya kwani hatuna mpango wa kushuka.

"Kwa sasa mashabiki waendelee kutupa sapoti bado kuna mechi za kucheza ambazo tunaamini kupitia hizo tutapata matokeo ambayo yatatutoa hapa tulipo," alisema.

# NAMUNGO HESABU ZOTE POINTI 3 ZA MWADUI LEO

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutinga hatua makundi ya Kombe la Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na kisha hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu FA Cup, Kocha Mkuu Namungo FC, Hemed Morocco, amesema nguvu zote sasa wanazielekeza katika kupambania pointi tatu kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mwadui FC leo.

Namungo ambayo katika michuano hiyo ya CAF iliitoa CD de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 7-5, imepangwa kundi moja na Raja Casablanca ya Morocco, Pyramids ya Misri na Nkana FC ya Zambia, na hatua hiyo ya makundi itaanzia ugenini dhidi ya Wamorocco hao Machi 10, mwaka huu.

Na kwa upande wa Kombe la FA, imeitoa Mbeya City kwa bao 1-0 ambapo sasa inasubiri kukutana na JKT Tanzania kwenye mechi ya hatua ya 16-bora mwanzoni mwa mwezi ujao.

**Leo itashuka katika Uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga kumenyana na Mwadui FC ikiwania alama tatu Ligi Kuu Bara kabla ya Jumamosi kukwea pipa tayari kwa safari ya Morocco kwenda kuivaa Raja Casablanca.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema wapo tayari kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mchezo huo dhidi ya Mwadui FC.

Alisema wachezaji wake wako fiti kwa ajili ya mchezo huo kuhakikisha wanapata matokeo kabla ya kwenda Morocco kuivaa Raja Casablanca.

"Tumejipanga vizuri kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya katika mechi dhidi ya Mwadui FC, wachezaji wako fiti kwa mchezo huo, utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata pointi," alisema Morocco.

Namungo ambayo imeshuka dimbani mara 16 hadi sasa, ipo nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 21, wakati Mwadui iliyocheza mechi 21 ikiburuza mkia na pointi zake 15.

**TAHADHARI...**




Baadhi ya wakimbiaji wa mbio za Kilimanjaro Marathon Kilomita 42 wakiwa wanaonyesha bango la kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona, wakati mashindano hayo yalipofanyika mjini Moshi mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam yamwongezea mkataba Kangwa*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC, imemwongeza mkataba wa mwaka mmoja beki wake wa kushoto, Bruce Kangwa ili aendelee kusalia kwenye kikosi hicho.

Kangwa, raia wa Zimbabwe amesaini mkataba huo Jumatanu mchana mbele ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa klabu hiyo, mkataba wa Kangwa ulikuwa unamalizika Agosti 2021, hivyo kwa kusaini mkataba huo mpya, utamfanya kusalia kwenye klabu hiyo hadi Agosti, 2022.

Mchezaji huyo ambaye ana uwezo wa kucheza pia winga ya kushoto, alijiunga na klabu hiyo Agosti 6, 2016 kwenye Ligi Kuu msimu wa 2016/17, akitokea klabu ya The Highlanders ya nchini Zimbabwe.

Klabu ya Azam imekuwa na utaratibu wa kuwaongeza mikataba wachezaji wake, mara tu inapokaribia kumalizika, tofauti na klabu nyingine ambazo husubiri mikataba iishie na kuanza kukimbizana na wachezaji, tena wakisikia klabu fulani zinamhitaji.

Hivi karibuni iliwaongezea mikataba nahodha wao, Aggrey Morris, Yakub Mohamed na Salum Aboubakar 'Sure Boy'.

Azam imeamua kubakisha wachezaji wake muhimu wakati huu ikiusaka ubingwa wa Tanzania Bara ikiwa kwenye nafasi ya tatu kwa pointi 37, lakini ikikabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Simba inayoshika nafasi ya pili kwa kupointi 45 na Yanga inayoongoza ligi na alama zake 49.

Michezo

Jumatano Machi 3, 2021

Nipashe



Hughes aipeleka Utd kwa Kane, Haaland UKURASA 22



Kikosi cha Simba kikiwa mazoezini kujiandaa na mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika. Jumamosi miamba hiyo ya Ligi Kuu Bara itashuka dimbani nchini Sudan dhidi ya Al-Merrikh. **PICHA: MAKTBA YETU**

# MIQUISSONE, ONYANGO NDANI KIKOSI CHA CAF

## Bao aliloifunga Al Ahly latangazwa kuwa bora, waifuata Al-Merrikh huku Gomes akisema...

**Na Mwandi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakikwea pipa leo kuelekea Sudan tayari kwa mechi yao ya tatu ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wachezaji wake wawili, beki wa kati Mkenya Joash Onyango na winga raia wa Msumbiji, Luis Miquissone majina yao yamechomoza katika kikosi bora cha wiki cha Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

**Mbali na kutajwa katika kikosi hicho bora cha CAF, pia bao la Miquissone alilofunga wakati Simba ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, limechaguliwa kuwa bao bora la wiki la michuano hiyo.**

Aidha, Simba, Waydad Casablanca ya Morocco anayoichezea Mtanzania Simon Msuva pamoja na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, zimetajwa kuwa timu tatu pekee zilizoshinda mechi zake mbili za mwanzo za makundi na kukalia usukani.

Kikosi hicho bora cha wiki cha CAF kinaundwa na kipa Moussa Camara wa Horoya AC, Hamza Mathlouthi (Zamalek), Mouad Hadded (MC Alger), Joash Onyango (Simba), Pape Ndiaye (Teungueth), Muaid Ellafi (Waydad Casablanca), Luis Miquissone (Simba), Kermit Erasmus (Mamelodi Sundowns), Themba Zwane (Mamelodi Sundowns), Obed Mayamba (AS Vita) na Ayoub El Kaabi wa Waydad Casablanca.

Kwa mujibu wa taarifa zilizolifikia Nipashe jana, kikosi cha Simba na baadhi ya viongozi wa timu hiyo, kinatarajia kuondoka leo saa 10:45 alasiri kuelekea Sudan kwa ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia, ambapo kitapitia Ethiopia na kupumzika kwa saa kadhaa kabla ya kuunganisha safari kuelekea Khartoum ambapo kinatarajiwa kufika saa 2:00 usiku tayari kwa maandalizi ya mechi yao ya Jumamosi dhidi ya Al-Merrikh.

Akizungumzia mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema anafahamu utakuwa mchezo mgumu, lakini anaamini watafanya vizuri katika mchezo huo na kwa upande wake hakufanya makosa kujiunga na timu hiyo yenye makao yake makuu mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam.

"Nina kikosi kipana, na wachezaji wangu wanauwezo wa kupata matokeo, ninafurahi kuwa katika timu hii, ninaamini tutafanya vizuri katika mechi yetu ijayo.

"Nafahamu itakuwa mechi ngumu, lakini ninawafahamu vizuri Al-Merreikh, ubora na udhaifu wao, ninaamini utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu wao watakuwa wanatafuta matokeo ya kwanza katika mchezo huo," alisema Gomes.

Kuhusu hali ya kipa wa Simba, Aishi Manula ambaye juzi aliumia katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania na kulazimika kukimbizwa Hospitali ya Kairuki, Mikocheni, Dar es Salaam, Daktari wa timu hiyo, Yassin Gembe, alisema yupo fiti na tayari ameruhusiwa kurejea nyumbani ambapo atapata mapumziko mafupi (jana) na leo atajiunga na wenzake tayari kwa safari ya kuelekea Sudan.

Kwa upande wa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Haji Manara, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuhusu hali ya kipa huyo aliyepoteza fahamu baada ya kugongana na straika wa JKT Tanzania, Danny Lyanga waliporuka juu kuwania mpira wa krosi.

"Amenihakikishia hali yake inaendelea vizuri, nimetoka kuongea naye muda si mrefu. Amepata matibabu mazuri Hospitali ya Kairuki. Tunawashukuru wote waliosimamia matibabu yake," alisema Manara.

# Yanga, Coastal vita nje, ndani ya uwanja

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union yenye makao yake makuu jijini Tanga, Juma Mgunda, ameanza kuitishia 'nyau' Yanga kwa kuieleza ushindi wa mabao 2-0 waliopata kwenye mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Ihefu FC ni salamu kwa miamba hiyo ya Jangwani jijini Dar es Salaam watakapokutana kesho.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka jijini Tanga jana, Mgunda alisema kwa sasa ameridhishwa na kiwango cha wachezaji wake hali inayompa matumaini ya kufanya vizuri watakapokutana na Yanga.

"Wachezaji wangu kwa sasa wamebadilika kwa kiasi kikubwa tofauti na ukilinganisha na siku zilizopita, makosa madogo madogo ambayo yalikuwa yamejitokeza ninaendelea kuyafanyia kazi ninaimani tutapata matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Mgunda.

Hata hivyo, wakati Mgunda akitoa kauli hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema anaamini mabadiliko ya mbinu atakazotumia zitampa matokeo chanya katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Mkwakwani kesho.

"Tunatazama namna gani tunaweza kupata matokeo chanya kwenye mechi zijazo, hilo ni la msingi kwetu, katika mbio za ubingwa, kikubwa kwa sasa ni kuwapa mbinu washambuliaji ili kuweza kuzitumia nafasi wanazotengeneza," alisema Kaze.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002